

# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

**Je,Wakristo Wanapaswa Kupiga Kura?**



**Je,Krismasi ni Sikukuu ya Kipepo ama ya Kibiblia?**

**Je,Mungu Anaweza Kutuacha wakati wowote?**

**Katika Toleo Hili:**

**2. Kutoka kwa Mhariri:** Je, Wakristo Wanapaswa Kupiga Kura? Wengine wanadai kwamba kupiga kura ni jukumu lao kama Wakristo? Biblia hufundisha nini?

**9. Je, Mungu Anaweza Kutuacha WAKATI WOWOTE?** Marehemu Colin Adair Anachambua Swali Hili.

**12. Kozi ya Biblia Somo la 10:** Unabii ni Uthibitisho wa Mungu! Wakati wengi wanapunguza ama wanadunisha unabii, kuna sababu inayofanya Biblia yako ijae na unabii.

**30. Vidokezi Ishirini na Nane vya Maombi Yanayofaa: Sehemu ya 5.** Je, ungependa kujifundisha jinsi ya kufanya maombi yako yafae zaidi?

**Jalada la Nyuma: Intaneti na Redio** Hii inaonyesha watu mahali pa kupata ujumbe wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).

**Kuhusu Jalada la Mbele:** Hizi ni picha za wagombea wa vyama viwili vya Afisi ya Rais ya Marekani. Picha ya Donald Trump imefanywa na Michael Vandon na ya Hillary Clinton imefanywa na Gage Skidmore.

Unabii wa Habari za Biblia inachapishwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG), 1036 W. Grande Avenue Grover Beach, CA, 93433. <http://www.ccog.org>

(c) 2016 Kanisa la Mungu Linaloendelea. Imechapishwa U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kuupokea gazeti hili, wasiliana na afisi yetu ya Grover Beach. Maandiko yamenukuriwa toka New King James Version (c) Thomas Nelson, Inc, Publishers, used by permission isipokuwa pale tu tumeelekezwa vinginevyo.

**Unabii Wa Habari za Biblia HUWEZESHWIA KWA MICHAJANGO YENU.**

**Mhariri Mkuu: Bob Thiel**

**Nakala/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel**

**Masahihisho: John Hickey; SBC Course Assister; Shirley Gestro.**

Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na vyanzo vya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa ni chanzo hakikutajwa; itakuwa ni kwa sababu inamaanika kwamba chanzo husika kiliachia picha iwe matumizi ya umma pasipo masharti yoyote).



**KUTOKA KWA MHARIRI MKUU,  
BOB THIEL;**

**Je,Wakristo Wanapaswa Kupiga Kura?**

Dunia ni mahali pagumu sana ambapo pamejaa shida za aina nyingi.Katika ulimwengu ambaa unaitwa wa demokrasia,wanasiasa wanafanya kampeni wakitusawishi tuwapigie kura ili watusaidie kuzitatau shida hizo.

Ulimwenguni pote,maswala ya uchaguzi na shida mara nyingi inahusu mambo kama uchumi,mazingira,uhalifu,uongozi wa kimataifa,ulinzi,na wingi wa matatizo ya kijamii.Viongozi wa jumuiya na mitazamo tofauti wanataka kutusawishi kwamba uchaguzi wa kundi lao ndio utakuwa wa muhimu sana kwa nchi.

Wengi wa viongozi hawa wanaleta dini katika kampeni.

**Je,Wakristo wanapaswa kupiga kura?**

Biblia inafundisha ya kwamba Wakristo wanapaswa kufuata mfano wa Yesu ( Wafilipi 2:5).Sasa ikiwa Yesu angekuwa mwananchi wa Marekani,je kwa hakika angepiga kura? Katika nchi zilizo na mifumo ya ubunge,je,angepiga kura kwa chama fulani ili achague waziri mkuu? Katika Marekani,wengine wanadhani ya kwamba Yesu angepigia chama cha Demokrasia,kwa sababu Wademokrasia wanaonekana kuwa na huruma kuliko Wa Jamhuri.Wengine wanahisi kwamba Yesu angepigia kura Wajamhuri kwa sababu wao huonekana na wengine kuwa "wahifadhi wa afya" ( Wanapinga utoaji wa mimba) kuliko Wademokrasia.Wengine,wakigundua unafiki katika pande zote za vyama,huisi kwamba Yesu angepigia mgombea wa chama kidogo kwa sababu ya utu wao ama mtazamo tofauti katika masuala tofauti.

Lakini Yesu angeenda kwa kituo cha kupiga kura na kupigia yeyote?

Demokrasia ilijulikana kabla wakati wa Kristo.Katika Ugiriki wa kale,wanaume wote walipaswa kupiga kura kwa masuala yote yaliyokabili jamii.Wagiriki walianzisha dhana ya demokrasia kwa Warumi.Warumi (ambao walikuwa wakipinga kiasi mtindo huo) walianza kurekebisha mfumo wa demokrasia unaoitwa Jamhuri.Katika jamhuri,mwakilishi

aliyechaguliwa anapaswa kupiga kura kwa ufanuzi wa matakwa ya watu.Marekani,demokrasia zingine za ulimwengu (na Uswizi kama linalooneka ni tofauti kwa sababu limeundwa kama umbo la Ugiriki),na hata makanisa mengine yameundwa kama la Rumi.

Watu wengi katika jamii ya Magharibi wanaonekana kuhisi kwamba aina ya demokrasia ndiyo aina nzuri ya serikali.Je,Mungu anaweza kukubali? Biblia inatuonya, "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu;Lakini mwisho wake ni njia za mauti" (Mithali 16:25).Inatuonya pia, "kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu" (Yeremia 10:23).

Katika Mwanzo 2:17 Mungu aliwaonya Adamu na Hawa wasile tunda la mema na mabaya.Lakini Adamu na Hawa hawakumsiliza Mungu.Baada ya kuwasiliza Shetani,wakaamua kwamba hawakua na haja ya kumsikiliza Mungu lakini wakaanza kujiamulia (Mwanzo 3:1-6).Hii ndio rekodi ya demokrasia ya kwanza katika tendo.

Hakuna mahali pengine pote katika Biblia ambapo Mungu ameidhinisha demokrasia.

Biblia inatuonyesha kwamba Mungu alichagua viongozi na kuwafanya wajulikane kwa watu wake.Kutoka kwa Henoko hadi Nuhu hadi Daudi mpaka manabii hadi Yesu na hata Mitume,hatujasoma mahali Mungu alihimiza demokrasia.

Kwa hakika kulingana na Biblia,demokrasia imelaaniwa.Wakati Samueli alikuwa kiongozi/mwamuzi mteule wa Mungu, watu wengi walitaka wawe na mfalme kama mataifa mengine.Hata hivyo ulionekana upinzani halali kuhusu uongozi wa Samueli.Mungu alimwambia Samueli kwamba watu wamemkataa Mungu lakini si Samueli (1 Samueli 8:1-9).Biblia inasema ilikuwa kitu kiovu mbele za Mungu kwamba watu wanahitaji serikali kama mataifa mengine majirani( 1 Samueli 12:17).

Biblia inasema kwamba Mungu huchagua ye yote anayetaka kuwa kiongozi na huyu ni "aliye mnyonge" (Danieli 4:17).Na kuhusu Marekani,yule atakayekuwa rais wa awamu unaokuja atawakilisha maangamizi ya kinabii kwa maana atachukua hatua zinazoongoza kwa utimizaji wa unabii.

Biblia inarekodi matukio ya viongozi wa dini ambao walidhani kwamba walikuwa wema kama viongozi ambao Mungu alichagua,lakini walikuwa na mawazo mengine.

Kwa mfano,Kora (ambaye alikuwa kiongozi wa dini na mlawi) alikuwa akipendekeza kupiga kura na aina ya serikali ya jamhuri ( ambao Marekani,kwa mfano,wanadai wanao).

Baada ya kukusanya wasaidizi 250 (ambao walikuwa viongozi wa jamii/Wawakilishi) aliwambia Musa na Haruni:

Ninyi inawatosha,kwa kuwa mukutano wote ni mtakatifu,kila mmoja mionganoni mwao,BWANA naye yu kati yao;n'nini basi kujitokuza juu ya mukutano wa BWANA? (Hesabu 16:3).

Mungu hakukubali na ukadiriaji wa Kora na akaamuru kifo kwa Kora na wafuasi wake (Hesabu 16:32).Wakati wengine walifkiria kwamba adhabu ya Mungu ni kali,Mungu akawaadhibu pia (Hesabu 16:49)..Basi,ni wazi kwamba Mungu hakuidhinisha kupiga kura kwa mfumo wa serikali ya jamhuri.

#### **Agano Jipyä Halikuidhinisha Demokrasia**

Ikiwa demokrasia ingeidhinishwa katika Biblia kwa Wakristo,kwa hakika ingeidhinishwa katika Agano la Kale.Njia za Ugiriki na Rumi ziliJulikana kwa upana.Katika Agano Jipyä tunaona vile Yesu anachagua mitume,baadaye manabii n.k kwa kujenga mwili wa Kristo (Waefeso 4:11,12).

Wakati nafasi ya Yuda ingechukuliwa (baada ya kumsaliti Yesu na kujinyonga),mitume hawakupiga kura,walifuata mfano wa Biblia ya kutekeleza mapenzi ya Mungu:

24 Wewe,Bwana,ajuaye mioyo ya watu wote,tuonyeshe ni nani uliyemchagua katika hawa wawili...26 Wakawapigia kura.( Matendo 1:24,26).

Kumbuka mitume hawakuamua kwamba walihitim kwa kuona moyo wa mtu.

Wengine wameandika kwamba mifumo tofauti ya demokrasia inakubaliwa kwa sababu wameamini maandiko mengine katika kitabu cha Matendo yanayodokeza hio.Maandiko hayo yanaonekana kutoka kwa Matendo 15.Katika Matendo 15 mitume wengi na wazee walikutanika kujadili tohara na waumini wa mataifa.Umati wa washauri walitumika kujadili suala.Wengine wanahisi kwamba kutumia ushauri unaonyesha demokrasia.Hata

hivyo,hakika kwamba umati wa washauri walitumika haibadilishi aina ya serikali ya Mungu.Katika Agano la Kale,tunasoma kuwa si kwamba Mungu amehimiza utendaji huo (Mithali 11:14),tunasoma pia kwamba Mungu Mwenyewe alitumia njia hio ( 2 Mambo 18:18-21);kwa hivyo uongozi mwingine wa kanisa uliofuata utendaji huo inaonyesha kwamba serikali ya Mungu unafanya hivyo kutoka kwa Agano la Kale na kuendelea.

Ni wa muhimu sana kugundua neno lingine ambalo limetajwa katika kitabu cha Matendo:

38 Basi sasa nawambia,Jiepusheni na watu hawa;waacheni kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa binadamu,itavunjwa, 39 lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja;msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu.” (Matendo 5:38-39)

Wanaopiga kura katika uchaguzi wa ulimwengu wanaamini ya kwamba wanajua kipengele cha mpango wa Mungu ambao hakuna njia ingine ya kibinadamu wanaweza kujua.

Lakini,tazama alichonena Mungu kwa Samweli,yule aliyechaguliwa na Mungu,wakati Samweli alifikiri alijua atakayekuwa mfalme wa Israeli:

6 Ikawa walipokuja,alimtzama Eliabu,akasema,Yakini masihi wa BWANA yupo hapa mbele zake.7 Lakini BWANA akamwambia Samweli,Usimtzame uso wake,wala urefu wa kimo chake;kwa maana mimi nimemkataa.BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo;maana wanadamu hutazama sura ya nje,bali BWANA huutazama moyo.(1 Samweli 16:6-7).

Samweli alichaguliwa na Mungu,na hakuja atakayechaguliwa na Mungu.Je,unafikiri unajua kuliko Mungu?

#### **Demokrasia Siyo aina ya Serikali ya Mungu**

Pia ni muhimu kugundua kuwa wengi wanaoamini kwamba Agano la Kale linaidhinisha demokrasia pia wanaamini kuwa serikali ya Mungu yajayo (kwa Ufalme wa Mungu) hautakuwa na demokrasia.Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba watakuwa viongozi juu ya mataifa kumi na mawili ya Isreali.

(Luka 22:30).Yesu alichagua wanafunzi,hawakupata nafasi zao kuitia kwa aina yoyote ya demokrasia (Yohana 15:16;6:70).Mungu,siye binadamu, hapo awali, alichagua Daudi awe Mfalme juu ya Israeli (Matendo 13:22) na pia amemchagua kuwa mfalme juu ya Israeli katika ulimwengu ujao (Yeremia 30:9).

Kwa ukweli, Yesu alisema kwamba Mungu Baba ametenga baadhi ya nafasi ya mamlaka katika ufalme wa Mungu ( Mathayo 20:23).Ujira katika ufalme, Yesu atawapa (Ufunuo 22:12);sio kwamba watu watachukua peke yao.

Demokrasia haitakuwa aina ya serikali katika Ufalme Wa Mungu.

Kwa nini?

Shida moja ya kupiga kura ni kwamba hakuna mtu anayefikiria vile Mungu anavyofikiria.

8 Maana mawazo yenu,wala njia zenu si njia zangu;asema BWANA(Isaya 55:8).

Yesu alipokuwa hapa duniani,alitangaza habari njema ya ufalme wa Mungu na kuwaambia watu watubu (Marko 1:14-15).Yesu alikataa kushiriki hata kwa uamuzi muhimu ya serikali akiwa hapa duniani (Luka 12:13-14).

Hata kama Yesu alifundisha kwamba tulipe ushuru (Mathayo 22:17-21),Alifundisha kwamba ufalme wake si wa ulimwengu huu (Yohana 18:36).Wakati ushuru unatakikana na serikali zote,kupiga kura haitakikani (kumbuka:kama serikali yako kisheria inataka upige kura,omba na ufanye angalau yanayotakikana).

Yesu aliwaambia wanafunzi wake waende ulimwenguni kote wahubiri habari njema kwa kila kiumbe (Mathayo 28:19,20).Yesu alisema kwamba wanafunzi wake wangekuwa katika ulimwengu huu lakini sio wa ulimwengu huu (Yohana 17:16).

Mtume Petro alielewa hili.Aliandika kwamba kuwa sehemu ya watu wa Mungu inafanya mtu awe sehemu ya taifa takatifu ( 1Petro 2:9).Mtume Paulo aliandika kwamba ulimwengu huu ni mbaya (Wagalatia 1:4).Biblia inaonya dhidi ya madhara ya kuwa sehemu ya mifumo ya ulimwengu huu na serikali zake na inatuambia tutoke kwake na tutengwe nao (Ufunuo 18:2-5).

Tazama yale ambayo Biblia yanafundisha yatatukia siku za mwisho na vile Wakristo wanatakiwa kufanya:

1 Lakini ufahamu neno hili ya kuwa siku za mwisho kutakuwako siku za hatari.2 Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe,wenye kupenda fedha,wenye kujisifu,wenye kiburi,wenye kutukana,wasiotii wazazi wao,wasio na shukrani,wasio safi,3 wasiopenda wa kwao,wasiotaka kufanya suluhu,wasingiziaji,wasiojizuia,,wakali,wasiopenda mema,4 wasaliti,wakaidi,wenye kujivuna,wampenda anasa kuliko kumpenda Mungu;5 wenye mfano wa utauwa,lakini wakikana nguvu zake;hao nao ujiepushe nao!( 2 Timotheo 3:1-5)

Kipengele hiki cha juu kinanikumbusha kuhusu viongozi wa kisiasa tofauti,hata wale wawili walio katika kinyang'anyiro cha Afisi ya rais ya Marekani.Kumbuka kwamba neno la Mungu haliimizi kupiga kura kama suluhisho kwa masuala haya katika siku za mwisho,lakini kujitenga na watu hao.

Paulo anasema kwamba Wakristo wawe wajumbe kwa ajili ya Kristo (2 Wakorintho 5:20).

Mjumbe ni nani? Kamusi ya Merriam-Webster ina ufanuzi yafuatayo:

1.Balozi rasmi;sanasana:wakala wa kidiplomasia mwenye cheo cha juu anaye kibali cha serikali ya kigeni au huru kama mwakilishi wa wakazi wa serikali yake ama mkuu au aliyechaguliwa maalum na mara nyingi kwa mazoezi ya kidiplomasia ya muda.  
2.Mwakilishi aliyeidhinishwa au mjumbe.

Kama wewe ni Mkristo wa kweli,wewe ni mwakilishi aliyeidhinishwa,balozi rasmi,kwa ajili ya Kristo!

Mabalozi mara nyingi huishi katika mataifa ya kigeni,ambapo yana uadui kwa imani yao.Mabalozi,hata kama wanaishi katika jamii zingine,hawahuksiki katika siasa za jamii wanamoishi.Kuna wakati watu wa Mungu watachukua serikali ya ulimwengu huu,lakini haujafika bado (Yohana 18:36),Danieli 7:17-

18).Utakuwa baada ya kurudi mara ya pili kwa Yesu (1 Wathesalonike 4:16,Ufunuo 11:15).

Kwa Wakristo,Petro aliandika:

9 Bali ninyi ni MZAO MTEULE,ukuhani wa KIFALME,TAIFA TAKATIFU,WATU WA MILKI YA Mungu,mperate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu:10 ninyi mliokuwa kwanza SI TAIFA la Mungu;mliokuwa HAMKUPATA REHEMA,bali sasa MMEPATA REHEMA.11 Wapenzi nawasihi kama mpitaji na wasafiri,ziepuhani tamaa za mwili zipiganazo na roho.12 Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa,ili,iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya,wayatazamapo matendo yenu mazuri,wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.13 Tiini kila kiamriwacho na watu,kwa ajili ya Bwana;ikiwa ni mfalme,kama mwenye cheo kikubwa,14 ikiwa ni wakubwa,kama wanotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda wema.15 Kwa sababu ndio mapenzi ya Mungu,kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu( 1Petro 2:9-15).

Wageni na wasiojulikana katika nchi hawapigi kura.

Sasa Biblia hajatajaka kura aliopiga Paulo (wakati alikuwa Sauli na kabla hajageuzwa).Kumbuka alichosema baadaye kuhusu hii:

9 Mimi pia nilikuwa nimeshawishika kwamba imenipasa kufanya yote yale yaliyowezekana kupinga Jina la Yesu wa Nazareti.10 Nami hayo ndio niliyofanya huko Yerusalem.Kwa mamlaka ya viongozi wa makuhani,niliwatia wengi wa watakatifu gerezani na walipokuwa wakiuawa,**nilipiga kura yangu kuunga mkono.** (Matendo 26:9-10).

Na wakati yaliyo juu haikemei kupiga kura,ni hapa tu neno” kura” ama “kupiga kura” imetumika katika Biblia.Na hayaonyeshi kwamba wenye bidii katika mambo ya kidini/wahafidhina/wenye huria hawapigi kura vizuri na wanaweza kufanya mambo mengi kinyume cha jina la Yesu Mnazareti.

### Je,Ulimwengu Huu ni wa Nani?

Wengi wanadai kwamba ni jukumu la Wakristo kupiga kura.

Wengi ambaao wanadai kuwa Wakristo hawaamini kwamba Ufalme wa Mungu ndilo jibu kwa yale yanayokumba taifa lao ama ulimwengu.Ingawa Biblia inasema Wakristo wanapaswa ”kutembea kwa imani,si kwa kuona” (2 Wakorintho 5:7),wanatoa sababu kwamba Mungu angetaka wafanye asiyeamuru.

Zingatia pia maandiko yafuatayo:

3 Lakini ikiwa injili yetu imesitirika,imesitirika kwa hao wanaopotea,4 ambaao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini,isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu( 2 Wakorintho 4:3-4).

Injili imesitirika kwa wale wanaohusika na siasa ya ulimwengu huu wa Shetani.

Kwa jinsi gani? Wanajiwakilisha kwa mamlaka ya Shetani ,si ya Mungu.Wanakosa kuchukua yafuatayo kwa makini:

3 Yafikirini yaliyo juu,siyo yaliyo katika nchi (Wakolosai 3:2).

Biblia pia inafundisha kwamba ”Yule joka wa zamani,aitwaye Ibilisi na Shetani....audanyaye ulimwengu wote” (Ufunuo 12:9).

Suluhisho la maovu ya ulimwengu ni kurudi kwa Yesu na kusimamisha Ufalme wa Mungu,sio viongozi wa kisiasa.

Wakati watu wanajitumbukiza kwenye siasa za ulimwengu na serikali zake,wanawakilisha dhana ya Shetani ya kuendesha vitu pasipo Mungu.Wengi wameweka matumaini yao sana katika uchaguzi kuliko Ufalme wa Mungu.

Je,Mkristo anapaswa kufanya nini?

Kumbuka maombi ya Yesu:

14 Mimi nimewapa neno lako;na ulimwengu umewachukia;kwa kuwa wao si wa ulimwengu,kama mimi nisivyo wa ulimwengu.15 Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu;bali uwalinde na yule mwovu .16 Wao si wa ulimwengu,kama mimi nisivyo wa ulimwengu.17 Uwatakase kwa ile kweli;neno lako ndilo ukweli ( Yohana 17:14-17).

Wakristo wa ukweli wamo ulimwenguni,lakini sio wa ulimwengu.Ulimwengu huu ni wa Shetani kulingana na Biblia.

Ukweli wa Biblia ni kwamba Wakristo hawapaswi kushiriki katika mifumo ya Shetani kwa kuwa siyo njia ya kuleta Ufalme wa Mungu.

### **Wanasiasa sio jawabu,kurudi kwa Yesu ndilo jibu**

Kumbuka mtazamo wa kawaida kuhusiana na uchaguzi wa rais wa Marekani wa mwaka 2012 kwa kuwa yana mawazo ya kutafakari kuhusu kampeni ya 2016 pia:

Wakati wamekabiliwa na mtanziko wa uwongo wa mchakato wa kisiasa wa demokrasia,watu wengi wanatulia "chini ya waovu wawili" kama aina ya ulegevu....

Kinyume cha shambulizi maarufu kwamba "wale wanaopiga kura pekee ndio wana haki ya kulalamika,"akili ya kawaida inatuongoza kwa hitimisho yenye ni kinyume.Ni wale tu ambao hawaleti uchokozi dhidi ya wengine wana haki ya kulalamika wakichokozwa.Wale,wanaogeza neno, "Lisha midomo inayowauma," linasimama imara,lakini kwenye sehemu mbovu.

Kura kwa maovu mawili ni sawa na kura ya uovu.( Daily Reckoning,October 19,2012)

Ni ya ajabu sana kuona chanzo cha kawaida ikileta hitimisho sawa kuhusiana na "mfumo wa demokrasia" na uchaguzi wa rais wa Marekani.Bila shaka, wengi wanaodai kuwa Wakristo wanaamini kwamba wanapaswa kupiga kura hata kama wazo hilo halijaidhiniswa katika Biblia.

Lakini kumbuka mawazo haya mawili:

20 Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema,na kwamba wema ni uovu (Isaya 5:20).

2 Usiandamane na mukutano kutenda uovu (Kutoka 23:2).

"Waovu wawili" sio mzuri.

Wacha tuangalie yale maandiko yanayofundisha kuhusu tabia za viongozi wa Mungu:

19 Sasa nisikilize mimi,nitakupa shauri,naye Mungu na awe pamoa nawe.Yapasa wewe uwe mwakilishi wa watu mbele za Mungu na ulete mashauri yao kwake.20 Uwafundishe amri na sheria,tena uwaonyeshe namna ya kuishi na kazi zinazowapasa

wao kufanya.21 Lakini uchague watu wenye uwezo mionganii mwa watu wote,watu wanaomwogopa Mungu,watu waaminifu wanaochukia mali ya dhuluma,uwateue wawe maafisa juu ya maelfu,mamia,hamsini na makumi. (Kutoka 18:19-21)

2 Roho wa BWANA alinena kupidia kwangu,neno lake lilikuwa ulimini mwangu.3 Mungu wa Israeli alinena mwamba wa Israeli akaniambia "Mtu anatawala watu kwa haki,wakati anapotawala akiwa hofu ya Mungu. (2 Samwel 23:2-3)

Wanasiasa wachache wanaidhinisha sheria na amri na hawana tamaa.Hata hivyo sio watu Wakristo wanapaswa kuidhinisha.

Tazama pia yafuatayo:

14 kama watu wangu,wanaoitwa kwa jina langu,watajinyenyekesha na kuomba na kuutafuta uso wangu na kuacha njia zao mbaya,basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao na nitaiponya nchi yao.(2 Mambo 7:14)

Toba ya kitaifa na maombi ndiyo Marekani linahitaji ama litapata adhabu ya Biblia (Habakuki 2:6-8;Danieli 11:39).Hayo pia ni sawa na mataifa yanayotumia Kiingereza kama U.K,Canada,Australia na Newzealand.Ulimwengu mzima unahitaji kutubu (Matendo 17:30).

Hata kama wengi wanaamini ya kwamba ni "jukumu la Wakristo" kupiga kura (hata hivyo jukumu hilo halijatajwa katika Biblia),wengine wanaonekana wamepuuzia unabii mwingine unaohusu viongozi wa siasa katika nyakati za mwisho:

12 Katika habari za watu wangu,watoto ndio wanaowaonea,na wanawake ndio wanaowatawala.Enyi watu wangu,wakuongozao wakukosesha,waiharibu njia ya mapito yako. (Isaya 3:12)

Ni wazi kwamba Isaya alitabiri kwamba kutakuwako na viongozi wa nyakati za mwisho ambao watakosesha watu.Hii ndio wanasisa wengi wanafanya kwa wazi au kinyume.

Wakati ni ukweli kwamba kama Mfalme wa Ninawi(Yona 3:5-6),viongozi wa kisiasa wanaweza kutangaza toba ya kitaifa baada ya watu kuanza kufunga,hakika ni kwamba tendo

hili halitiliwi maanani na kuzingatiwa na wengi wao,wacha hata kufanya.Inaonekana kwamba hili haliwezi kufanyika( Pengine baada ya uharibifu unaotabiriwa kutokea).

Mungu ataamua anayetaka acae katika Afisi mbalimbali,na huyo mara nyingi siye mtu "mzuri":

17 Hukumu hii imekuja kwa agizo la walinzi,na amri hii kwa neno la watakatifu,kusudi walio hai wapate kujuu ya kuwa Aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu,naye humpa amtakaye,naye humtawaza juu yake aliye mnyonge. (Danieli 4:17)

Kwa kupiga kura,mtu anaweza kupiga kura dhidi ya mapenzi ya Mungu.Watu wa Mungu hawataki wapatikane kumpiga Mungu vita .(Matendo 5:39)

Mara moja,katika miaka ya 1970,nilipiga kura katika uchaguzi.Lakini kwa sababu zingine,sikumpigia kura mwanasheria mkuu.Ningepigia kura afisi hii,ningempigia aliyeshinda-mtu ambaye alikuwa na mashtaka mengi dhidi ya Kanisa la Mungu ambalo nilishiriki mnamo mwisho wa miaka ya 1970.Kwa dhahiri,singeefanya tendo hili kwa kusudi,lakini nafurahi kwamba sikusaidia kuwezesha yule aliyelipinga Kanisa la Mungu (na hiyo ndiyo afisi sikuipigia kura wakati huo) Tazama pia maoni yanayotatiza kutoka kwa kumbukumbu la kawaida linalotetea demokrasia:

Kampeni zote za kisiasa zinadanganya na kupoteza.Twajua wote,na ujuzi huu "umeokwa kuwa keki," inavyosemekana,ukifika wakati wa kutathmini wagombea.(Bookman J.GM on Romney: "Campaign politics at its cynical worst." Atlanta Journal Constitution,October 31,2012)

Mgombea ye yote hafai adanganye na kupotosha.Na wakati sikubaliani na kauli kwamba wote wanadanganya,ukweli ni kwamba si tabia za kiungu kudanganya ama kupotosha,na hiyo siyo kwamba inaonyesha hawaungwi mkono pekee ,lakini pia haiungu mkono utaratibu wa demokrasia wa kisasa. Biblia inaonyesha kwamba binadamu,bila Mungu hawawezi kutatua shida zao.Yesu atarejea na hawezikuwa Mfalme wa wafalme ambaye amechaguliwa na watu ( Ufunuo 17:14).Shida zote wanadamu wamekumbana

nazo zitasuluhishwa kwa kurudi kwake Yesu na kuanzisha Ufalme wa Mungu:

3 Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kitu cha enzi ikitisema,Tazama,maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu,naye atafanya maskani yake pamoja nao,nao watakuwa watu wake.Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.4 Naye atafuta kila chozi katika macho yao,wala mauti haitakuwapo tena;wala maombolezo,wala kilio wala maumivu hayatakuwapo tena;kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.5 Na ye ye aketiye katika kile kitu cha enzi akasema,Tazama naya fanya yote kuwa mapya.(Ufunuo 21:3-5)

Haijalishi mgombea ye yote anayechaguliwa katika serikali ya kimwili,viongozi wa kisiasa hawataleta yaliyo juu hapo.

#### **Ni nini Wakristo Wanafaa Wafanye Kuhusu Viongozi?**

Kama Wakristo hawapaswi kupiga kura,tuwafanyie nini viongozi?

Waombee!

Kumbuka alichandika Paulo:

1 Basi,kabla ya mambo yote,nataka dua,na sala,na maombezi,na shukrani,zifanyike kwa ajili ya watu wote; 2 kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka,tuishi maisha ya utulivu na amani,katika utauwa wote na ustahivu.3 hili ni zuri,nalo **Iakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu;**(1 Timotheo 2:1-3)

Kumbuka kwamba inafaa tuombee viongozi wa ulimwengu na wenye mamlaka juu yetu ili tuishi maisha ya utulivu.Hakuna kupiga kura kumetajwa ambao wengi wanassema ni "jukumu la Mkristo"....maombezi kwa viongozi yanafaa.

Pia inafaa tuombee:

14 Mapenzi ya Bwana na yatendeke (Matendo 21:14).

Vile vile,Yesu alifundisha:

7 Nanyi mkiwa katika kusali,msipayuke-payuke,kama watu wa mataifa;maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi.8 Basi msifanane na hao;maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi

hamjamwomba.9 Basi salini hivi;Baba yetu uliye mbinguni,jina lako litukuzwe,Ufalme wako uje,10 Mapenzi yako yatimizwe,hapa duniani kama huko mbinguni (Mathayo 6:7-10).

Na hayo,naamini yanafaa yawe aina ya maombi Wakrito wapaswa kuwa nayo kuhusu uchaguzi.Wafuasi wa Mungu wa ukweli pia wanaambiwa:

**5 Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote**,Wala usizitegemee akili zako mwenyewe,6 Katika njia zako zote mkiri yeye,Naye atayanyosha mapito yako.7 Usiwe mwenye hekima machoni pakoi;Mche BWANA,ukijiepusha na uovu.(Mithali 3:5-7)

Kupiga kura anayeendeleza maovu,kama utoaji mimba (kama Hillary Clinton) na "nchi kwanza," kwa kupuuzia amri ya kwanza,kama ilivyo hali ya Wajamhuri (kama Donald Trump) si kitendo cha Mkristo.

Watu wengi,hata hivyo,hawajatosheka na himizo la Biblia kwamba tumtumainie Mungu ili achague viongozi wa kisiasa.Jambo hili si geni (1 Samweli 8:6-7).

Na wakati sielewi hakika kwamba watu wanahisi kuwa wanafaa kufanya zaidi,watu wanashahau kwamba Mungu aliongoza Yeremia kuandika:

23 Ee BWANA,najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake;kuelekeza hatua zake si katika uwemo wa mwanadamu (Yeremia 10:23).

Pia tazama vile Hosea aliongozwa kuandika:

12 Basi,mrudie Mungu wako;shika fadhilli na hukumu;ukamngoje Mungu wako daima (Hosea 12:6).

Itakuwa ya muhimu kuonyesha kwamba Yesu alipendekeza kuwa watu watachukua mambo mikononi mwao wakifikiri wanahudumia Mungu (Yohana 16:2).Na wakati neno hili linaashiria uuji,kanuni bado ni kwamba mtu hafai akiuke alichoagiza Mungu na kukitakasa anachofikiria kama matakwa ya Mungu.

#### **Je,Wakristo Wanapaswa Kupiga Kura?**

Wakristo hawapaswi kuwa sehemu ya ulimwengu huu ( Ufunuo 18:1-4),lakini wanatakiwa wawe mabalozi wa Yesu (2 Wakorintho 5:20).Wakristo wa kweli "

wanazishika amri za Mungu,na kuwa na ushuhuda wa Yesu" (Ufunuo 12:17).

Yesu hakupiga kura wakati alikuwa hapa duniani.Wajumbe wa Yesu wanapaswa kufuata uongozi wa Yesu Kristo na Biblia lakini si kupiga kura.

Biblia haijaamrisha kupiga kura au demokrasia.Biblia inakemea zote,kupigia mtu binafsi au wa jamhuri.

Biblia inafundisha kwamba Wakristo wanafaa kuwaombea viongozi wao wa serikali (1 Timotheo 2:1-3) haifundishi ya kwamba kupiga kura ni jukumu la Wakristo.

Wale wanaojali kuhusu uchaguzi wa viongozi wa nchi zao wanafaa kuomba (na ikiwezekana kufunga) ili "mapenzi ya Bwana yatimike" (Matendo 21:14).

## KUACHWA



### Je,Mungu Anaweza Kutuacha WAKATI WOWOTE ?

Na Colin Adair

Hili lilichapishwa awali na Jarida la Habari Njema la Kanisa la Mungu Ulimwenguni pote mnamo Oktoba-Novemba 1979.Mimi,Bob Thiel,nilikutana naye mara moja mnamo 1997 au 1998.

Mkafiri,ili atekelze imani yao kuwa hakuna Mungu,ataonyesha hali ya kutisha katika ulimwengu na kusema: "Ona,hakuna mungu.Na hata kama unaweza kunishawishi kuna mmoja,naweza kusema kwamba amesahau na kuacha binadamu.'Sisi wa Kanisa la Mungu twajua kuwa wazo hili si kweli.Twajua kuwa Mungu yuko na ana mpango na anaufanya kazi hatua kwa hatua.Hajatuacha.

Na bado kuna wakati ,watu wake,wanahisi kwamba Mungu ametuacha,sanasana mambo yakienda mrاما,wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa na majoribu yanakosa kukoma?

#### Tabia ya binadamu ni kutia shaka

Shaka kama hizi lazima ingeingia mawazoni mwa watu wengine wakuu wa Mungu,hata kama Mungu alikuwa akifanya kazi nao,kwa sababu ni tabia ya binadamu.

Nuhu angeangalia nje na kuona tandiko la maji na kustaajabu kama Mungu angemkumbuka.Nuhu na familia yake walitoka mahali pa usalama baada ya mwaka mmoja na siku 10.Hiyo ni muda mrefu ukifungiwa ndani ya safina.Lakini wakati shaka iliingia katika mawazo yake angekumbuka ahadi za Mungu,na kwa hakika,Mungu alimkumbuka Nuhu (Mwanzo 8:1).

Abrahamu,baba wa imani,hakuwa mkamilifu kiasi cha kwamba hangekumbuka wakati ambapo alihisi kusaulika na Mungu.Baada ya kuambiwa kwamba angekuwa na mtoto na mrithi na mke wake,Sara,subira yake ikadidimia.Labda alisema kwamba Mungu amemsahau ama amemwacha?

Wakati nafasi ilipatikana atolewe gerezani,na ikaonekana kuwa Mungu mara ya mwisho anafanya kitu kuhusu hatma yake,rafiki yake

mnyweshaji,ambaye aliahidi kuongea na Farao kwa niaba yake,alimsahau haraka!

Kikwazo kama hiki kingemvunja moyo mtu yeyote.Yosefu,kama binadamu lazima angekuwa na shaka akilini mwake kuhusu uhusiano wa Mungu.Lakini ndani ya moyo wake alibaki akiamini kuwa Mungu alikuwa naye na matukio yaliyofuata yaliidhinisha kwamba Mungu hakumwacha hata dakika moja.

Pengine mfano wa ajabu wa mtu ambaye alioneckana kuwachwa na Mungu ni Ayubu.Baada ya kupoteza mifugo yake,watumwa na watoto katika mfululizo wa majanga ambayo yanafanana na mashambulizi ya kisasa ya kijeshi,alisema, "Mimi nilitoka tumboni mwa mama yangu nili uchi,nami nitarudi tena huko uchi vilevile;BWANA alitoa,na BWANA ametwaa;jina la BWANA na libarikiwe." (Ayubu 1:21)

Aliuja ilikuwa kazi ya Mungu na bado Mungu alikuwa naye.Wakati huu wa kujaribiwa,mtazamo wa Ayubu bado ulikuwa wakuigwa.Mstari wa 22 unatuambia kwamba katika haya yote Ayubu hakufanya dhambi.Pengine watu wengine wenye nguvu kidogo kuliko Ayubu,wangemshtaki Mungu kwa kuwaacha na kutolinda mali yao na familia zao.

#### Mfano wa Mfalme Daudi

Pengine mfano bora tunao kuhusu tabia hii ya asili ya mwanadamu ni ya Mfalme Daudi.Mara nydingi alikuwa kwa huzuni sana na kuhisi kwamba Mungu amemwacha.Na tazama vile alikumbana na shaka hii:

Katika Zaburi 13:1-2,twasoma:

"Hata lini utanisahau,hata milele?Hata lini utanificha uso wako? 2 Hata lini nifanye mashauri nafsini mwangu,Nikihuzuniya moyoni mchana kutwa? Hata lini adui yangu atukuke juu yangu?"

Alikuwa kwa asili ya binadamu akimlilia Mungu na maana aliposema kwamba Mungu amemwacha.Lakini hata wakati shaka iliingia katika mawazo yake alizima na mawazo mazuri kuhusu upendo wa Mungu kwake.Mstari wa 5,

" Nami nimezitumainia fadhili zako;Moyo wangu na uufurahie wokovu wako."

Daudi alijua kwa undani kwamba Mungu katika wakati wake mwema atamwokoa na kuwa hakuachwa.Kumbuka tena wakati mwingine ambapo Daudi alitia shaka kiasi:Zaburi 42:9-10:

“Nitamwambia Mungu wangu,mwamba wangu,Kwa nini umenisahau? Kwa nini nitakwenda nikhuzunika,adui wakinionea? 10 Watesi wangu hunitukana mithili ya kuniponda mifupa yangu,pindi wanaponambia mchana kutwa,Yuko wapi Mungu wako?

Sio kwamba Daudi alistaajabu mahali Mungu yupo peke yake,lakini maadui wake walimdhihaki waliongeza kidonda kwa majaribu yake na dhihaka zao.Lakini Daudi hakuruhusu fikra mbaya ziingie katika mawazo yake.

Kujua kwake Mungu na upendo wake kwa Mungu kilichukuwa nafasi katika wazo lake wakati wa shida.Alikosoa fikra zake.Mstari wa 11, “ Nafsi yangu,kwa nini kuinama,Na kufadhaika ndani yangu? Umtumaini Mungu;Kwa maana nitakuja kumsifu,Aliye afya ya uso wangu,Na Mungu wangu.”

Wakati asili ya kibinadamu ya Daudi ilienda chini,alifikia hatima ya mawazo yake na kumkumbuka uaminifu wa Mungu na kujua kuwa hajaachwa naye.

#### Nani Amemwacha Mwingine?

Wakati tumeanza kufikiri kwamba Mungu ametupa kisogo,inatakikana tujichunguze na kuona ni nani amwemwacha mwingine.Pengine Mungu hajibu maombi yetu na kutuokoa kutoka kwa majaribu yetu kwa sababu tumemwacha.

Ni kwa njia gani tunamwacha na kusahau Mungu? Njia ya kawaida sana ni kutotii sheria zake.Mithali 3:1 inaonya,

“Mwanangu, usisahau sheria yangu,Bali moyo wako uzishike amri zangu.”

Mstari wa 6,

“Katika njia zako zote mkiri yeye,Naye atanyosha mapito yako.”

Mungu atanyosha mapito yetu ikiwa tutaendelea kuwa naye na kumtii.

Je,tunatunza Sabato vizuri? Je,tu waaminifu kutoa zaka? Je,tunatunza Sikukuu na kuwa na mpango wa kuhuduria Sikukuu ya Makambi kwa kuhifadhi zaka ya pili? Je,tunatii serikali ya Mungu,tukijua kwamba serikali yake i hapa

ndani ya Kanisa,na Mungu anatutazama mtazamo wetu na ngazi ya huduma?

Njia nyingine ya kumwacha Mungu na kupuuzia maombi na kusoma Biblia.Mithali 8:33-34: “Sikieni mafundisho,mpate hekima,Wala msiikatae. Ana Heri mtu yule anisikilizaye,akisubiri sikuzote malangoni pangu.” Usilaumu Mungu kwamba amekuacha wakati umempa kisogo.

Je,unaomba sikuzote? Luka 18:1,

“Akawaambia mfano,ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote,wala wasikate tama.”

Pengine unaomba mara moja,na usipopata jawabu haraka,unaanza kufikiri kwamba Mungu hakisikia ama amesahau dua yako. Lakini atajibu kwa njia yake na wakati wake.Tunapaswa kumkumbusha na tusubiri tukingoja.Usifikiri Mungu amekuacha na hana haja tena kujibu maombi yako.

#### Usidharau Maonyo

Njia ya muhimu ya kumwacha Mungu na mara nyingi imepuzuliwa mbali sana ni kutotii ushauri.Mithali 1:24-25,

“Kwa kuwa nimeita,nanyi mkakataa;Nimeunyosha mkono wangu,asiangalie mtu;25 Bali mmebatilisha shauri langu,Wala hamkutaka maonyo yangu”

Mistari ya 30-33;

“Hawakukubali mashauri yangu,Wakayadharau maonyo yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao,Watashiba mashauri yao wenyewe.Maana kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua,Na kufanikiwa kwao wapumbavu kutawaangamiza.Bali kila anisikilizaye atakaa salama,Naye atatulia bila kuogopa mabaya.”

Shauri hili linatufikia namna gani?Mara nyingi ni kupidia kwa huduma ya Kanisa la Mungu.Inawezeshwa kwa njia mbili.Ya kwanza ni kupidia mafundisho na ya pili ni kupidia kwa ushauri wa mtu binafsi.

Tunaanza huduma ya kanisa kwa kuomba Mungu aongoze mnenaji.Lakini kama mshiriki,unafikiri mhudumu anakupatia maoni yake?Je,unakosoa mafundisho baadaye?

Wahudumu wa kweli wa Mungu wanenena mapenzi ya Mungu,siyo maoni yao.Hapana,siyo kwamba hawana dosari,na wanaweza kufanya makosa na

wanafanya,lakini ujumbe unaosikia kwa jumla,himizo,unalopokea hutoka kwa Mungu kupidia kwa mtumishi wake.

Watumishi wake wanakupatia uelewa wa mapenzi yake,ambayo yamejengwa kwenye msingi na mafundisho ya Mungu yanayodhibitika,ambao washirika wanao kama msingi wao (Waebrania 6:1-2).Hapa ndipo Mungu hushauri watu wake.Hakikisha hujapuuzia kwa sababu kufanya hivyo kunamaanisha kumwacha ushauri wa Mungu. Sasa haitakikani tulaumu Mungu wakati tumekosa,tukidhani hajali kamwe.

Tazama anachosema katika Isaya 49:14-16 kuhusu tabia hii. "Basi Sayuni (Kiroho ni Kanisa)alisema,YEHOVA ameniacha,Bwana amenisahau. Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye? Naam,hawa waweza kusahau lakini mimi sitakusahau wewe. Tazama nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu;kuta zako ziko mbele zangu daima.

### Kwa Mfano Wake

Sisi ni kazi maalum ya Mungu,uumbaji wake wa kiroho.Mungu amepanga kuumba wengine kwa mfano wake.Haachi alichoanza.Anaikamilisha.Na Kristo aliye Kuhani wetu Mkuu,anajali kwamba tufaulu.Hawezi kuacha chanzo chetu.Yohana 10:27-30:

" Kondoo wangu waisikia sauti yangu;nami nawajua,nao wanifuata.Nami nawapa uzima wa milele;wala hawatapotea kamwe;wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu.Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote;wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.Mimi na Baba tu mmoja.

Pamoja wanahuksika kwa kuleta watu wote waliochagua katika familia ya Mungu.Yohana 6:39,

"Na mapenzi yake aliyenipeleka ni haya,ya kwamba katika wote alionipa nisimpoteze hata mmoja,bali nimfufue siku ya mwisho."

Baada ya kutoa ahadi hii kwake na kwa Kristo,je,atatuonyesha kisogo na kujishughulisha na kazi nyingine muhimu kuliko uzazi wake? Hakuna kazi nyingine muhimu wakati huu katika mawazo ya Mungu! Yesu Kristo anatuhitaji tufike katika Ufalme wa Mungu.Yohana 17:24,

"Baba,hao ulionipa nataka wawe pamoja name po pote nilipo"

Ni huzuni ulioje kuona waliokuwa ndugu kwa imani wakihi kwamba Kristo ameacha watu wake,Kanisa lake.Anatuambia kuwa atakuwa nasi hadi mwisho wa dahari (Mathayo 28:20) Ni aibu ilioje wakati maadui wa Kanisa la Mungu hawagundai haya kabla hawajainua mikono yao dhidi ya Kanisa.Kila mara wanapata kwamba hakika Yesu yuko pamoja nasi na hajatuacha.Wanagundai kuwa ni ngumu sana kupigana na Mungu.

### Tafuta Mungu Kwanza


Kadri tunavyozidi kumtafuta na kuishi naye,tunadhamana kwamba Mungu hatatuacha.Luka 12:31-32: "Basi utafuteni ufalme wa Mungu,na hayo mtaongezewa.Msiogope enyi kundi dogo;kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme."

Hakuna kitu cha kuogopa.Wakati mambo hayaendi vizuri,Mungu anajua.Anafahamu vizuri na ana kusudi kwa jambo hilo.

Inatupasa tuhakikishe hatujasahau Mungu.Wakati tumejaribiwa kufikiria namna hiyo,tujaribu kukumbuka Daudi na kujikumbusha ahadi kuu ya Mungu,inayopatikana katika Waebrania 13:5,

"Msiwe na tabia ya kupenda fedha;mwe radhi na vitu mlivyo navyo;kwa kuwa ye ye mwenyewe amesema,Sitakupungukia kabisa,wala sitakuacha kabisa."

**KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA**  
**Somo la 10:Ishara ya Unabii Uliotimia**



Bob Thiel,Mhariri Mkuu  
Imechapishwa 2016 na Kanisa la Mungu

Utangulizi:Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na Kozi kwa Mawasiliiano iliyohaririwa mwaka 1954,iliyoanza chini ya usimamizi wa hayati C.Paul Meredith kupitia Kanisa la Mungu la Redio.Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebak yalivyo).Kadhalika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatifu,pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali.

**UNABII NI THIBITISHO LA MUNGU**

Imekadirwa kwamba karibia 1/3 ya Biblia ni unabii(Kuna makadirio tofauti,lakini hatuwezi kujua mpaka ufufuo wa kwanza,ambao pia ni unabii.Wakati wengi wanaodai kuwa Wakristo wanadai kuamini sehemu zingine za Biblia,na idadi kubwa isiyohesabika wanadai kuamini yote,wengi wanadai kuwa wana ufhamu mdogo wa unabii.Wengi wanaridhika kwa kupuuzia yanayofundishwa na Biblia.Na mionganoni mwa wanaodai kuthamini neno la unabii,wengi wao hawaelewi kipengele chake. Katika hisia ,VICHWA VYA HABARI vinavyotatiza vya mwongo mmoja au mingi TAYARI VIMEANDIKWA MAPEMA-katika unabii! Na bado viongozi wa serikali-na watu wengi hawavutiwi nayo!

**Habari za Kesho Zimeandikwa Leo**

Habari za JANA TAYARI ZIMEANDIKWA katika UNABII wa Biblia! Iliandikwa KITAMBO kabla ya

matukio yatakayotetemesha dunia ya ghadhabu ya Mungu kutokea-lakini watu wengi leo wanapuuzia "kinachouzwa sana" ulimwenguni.

Wachache wanaamini kwamba BIBLIA INAMAANISHA INACHOSEMA-na bado wachache HAWAELEWI unabii wake!

Wengi wangesema HAIWEZEKANI kwa wanadamu-kwa miaka 2600 iliyopitakutazama siku zijazo na KUTABIRI kitakachotukia kwa MATAIFA YOTE MAKUBWA KATIKA SIKU ZETU.

Wataalam wa hali ya hewa mara nyingi wanashindwa kutabiri hali ya hewa hata kwa masaa 24 au 48 yanayokuja.Ni nafasi gani mtu anaweza kuwa nayo ya kutabiri majanga maalum yatakayotokea kwa mataifa makuu kama Marekani? Kwa mataifa yaliyotoka Uingereza? Kwa Ujeruman?Urusi? Ama China? Na kupata kwamba unabii unatimika-isipokuwa WAMEONGOZWA NA MUNGU?

**Unabii Wa Ajabu**

Watu kama hao walikuwa! Na unabii huo ulifanywa!

Manabii ambao walitabiri hatma ya mataifa leo-ambao walitabiri kitakachotendeka pengine miaka 15 ya maisha yetu-PIA alitangaza miaka 2600 iliyopita matukio YASIOONEKANA YA AJABU,SI YAMKINI,HATA HAYAWEZEKANI ambayo yatapata mataifa makuu na miji ya mataifa ya ULIMWENGU ZAMANI SANA.

NABII HIZO ZILITOKEA! Zilitokea karne nyingi baadaye-zilitimika SAHIHI VILE MANABII WALITABIRI! Na THIBITISHO utapata katika somo hili!

Ikiwa Biblia ilitabiri siku zijazo ya mataifa yote yanayoongoza miaka 2600 iliyopita-Misri,Ashuru,Babeli,Uajemi,Ugiriki,Utarwala wa Rumi na unabii huo ukatimilika,BASI NI WAKATI UNAOTAKIKANA TUANZE KUTAHADHARI NA KUANGALIA UNABII WA BIBLIA ili tuone zinazofunua kuhusu mataifa LEO-na kuona zinazotabiri kwa watu wetu.KWA SABABU TUMEWEKWA PAMOJA KATIKA UNABII WA BIBLIA!

LEO Mungu anafanya uwepo wake ujulikane kwako kwa kuonyesha kwamba Neno lake takatifu-Biblia Takatifu,inaweza kutegemewa.

#### **Unabii ULIOTIMILIIKA Unaonyesha Nini?**

Je,ni jambo la busara kuamini MUNGU? Ama Mungu ni hadithi,uvumbuzi wa ujinga wa ushirikina uliopita? Na unabii wa Biblia ni wa ukweli ama visio vya ujanja vya Wayahudi walioishi zaidi ya miaka2,000 iliyopita?

Katika ulimwengu wa vita na uwongo,swali la kuwepo kwake Mungu na msukumo wa unabii unatatiza idadi kubwa ya watu.Wengi wanasema wanataka UKWELI!Wanadai wamepitia katika kupumbazwa-wamepitia kwa HEKAYA katika nafasi hizo kama UKWELI,walikupuuzia bila kujua yanayofundishwa.Wengi wanataka kujua! Wanahitaji uthibitisho!

#### **UNATAKIKANA UHISI VILEVILE KUHUSU UKWELI!**

Mahali pa kuanza uchunguzi wa ukweli ni kwa MUNGU Mwenyewe.Inafaa uwe UTAFUTAJI MUHIMU katika maisha yako unaohitajika na KUTAFUTA THIBITISHO la kuwepo kwa Mungu na uongozi wa neno la unabii-Biblia Takatifu! UNABII uliotimilika ni THIBITISHO la KUWEPO KWA MUNGU MWENYEZI.Ni THIBITISHO la UONGOZI MKUU WA BIBLIA.Ni THIBITISHO kwamba Biblia ni UFUNUO ya ukweli kutoka kwa Mungu Mwenyezi ambao hatungetambua ama kujua mapema.

Aliyetia msukumo nyuma ya unabii wa Biblia ALIJUA MIAKA 2600 ILIYOPITA VILE HALI YA ULIMWENGU UTAKAVYOKUWA LEO.-hali ya kimataifa ya Marekani,Urusi,China na mataifa yanayoongoza duniani.Mungu aliyeongoza alijua miaka elfu iliyopita kitakachofanyika katika siku zijazo!

Ni kimantiki,sasa kuamini Mungu ambaye alitengeneza MPANGO wa dunia ujulikane miaka mingi mapema.

#### **Biblia Inathubutu Kutabiri Yajayo!**

Watu wengi WANAOGOPA unabii wa Biblia!Wanaogopa kwamba wakichunguza unabii uliotimilika,WATAPATA THIBITISHO la msukumo mkuu wa maandiko!

Kama unabii haujatimilika,basi wasioamini wangkuwa na thibitisho kwamba Biblia ni udanganyifu.Biblia ingesimama kama kitu kibaya cha mzaha ambacho kimechochewa juu ya ulimwengu mwenye udanganyifu wa

kidini.LAKINI UNABII UMETIMILIIKA na thibitisho liko katika somo hili la Kozi ya Biblia! Hapa kuna kitabu-Biblia Takatifu-kinachodhihaki wasioamini kwa kujivunia kutabiri katika kurasa zake historia za siku zijazo za ulimwengu huu! Mungu anataka tuangalie ndani ya kurasa zake na kuthibitisha msukumo wake usiopingika!

Twaweza kosa kuwa MAKAFIRI,WASIOAMINI AMA WAKANAJI.Twaweza kukosa KUDHIHAKI Biblia Takatifu.Lakini tunaishi katika wakati wa UZEMBE na SHAKA.Watu wachache mno wanataka kutumia akili vizuri KUTHIBITISHA kama UNABII Umetiwa msukumo na Mungu.Wachache bado WANATETEMEKA wakisikia unaonena unabii huu,ama wanazingatia kama wenyе UNA MAMLAKA! Watu wengi ambao wamesoma zaidi,kama watu wa Sayansi,WANADHANI kwamba Biblia sio Ufunuo usiodanganya wa Mungu Mkuu. Wanadhani hivi bila THIBITISHO LA KISAYANSI ambayo wanahitaji kwa vitu vinavyoenekana.Wanachukua kama MZAHA kwamba unabii,ambao ni thibitisho la Mungu,si wa ukweli –lakini hawajapata kuchunguza.HAWATAKI KUJUA UKWELI WA MAMBO HAYA!

Wengi “wenye msimamo mkali,” kwa upande mwininge,wanachukua kama mzaha kwamba maandiko ni Neno la Mungu-lakini wanakanusha MAMLAKA yake juu ya maisha yao.Kwa hivyo ,wao pia,HAWAELEWI UNABII WAKE.Wanashuhudia Babeli ya mafundisho ya machafuko kuliko unabii wa Biblia.Ni ngumu sana wakubali masuala mengi ya unabii.Wanatangaza Kristo lakini wanakana ujumbe wake.

Ni wakati ambapo unatakikana tuache kuchukua maswali haya muhimu kama mzaha. “ msitweze unabii;(JARIBUNI MAMBO YOTE;LISHIKENI LILIO JEMA)” (1 Wathesalonike 5:20-21).

#### **Utahakikishaje Maandiko?**

Kristo mwenyewe ametajwa katika Biblia akisema, “ Na maandiko HAYAWEZI kutanguka” (Yohana 10:35).Lakini yanaweza kutanguka? Je,umewahi kujaribu kutangua? Je,Umewahi kuweka unabii wake katika JARIBIO-na kuthibitisha.

Je, imefika wakati ambapo tunaweza kuanza kutafuta thibitisho kwa njia moja au nyininge?

Watu wengine wanafikiri kwamba njia pekee ya kuthibitisha msukumo wa Biblia-na hata unabii wake-ni kwa njia ya miujiza ya Yesu.Lakini makafiri hawaamini kama miujiza hio ilifanyika-hata kama ushuhuda wa kihistoria wa Wayahudi wasioongoka na wapagani wanakubali kwamba Yesu ALITENDA miujiza hio.Makafiri wanaweza kutufanya tuamini kwamba hata maadui wa Yesu walipumbazwa kufikiri kwamba miujiza ilitendeka.Makafiri wanataka uthibitisho ambao wanaweza KUCHUNGUZA LEO!

Kwa haraka,wengi wanadhani kuwa MAOMBI YALIYOJIBIWA ndiyo thibitisho kubwa ya msukumo.Lakini makafiri hawajakuwa na maombi YALIYOJIBIWA.Hawajaamini kama kuna aliyejibiwa maombi. "Ni hali tu ambapo watu wa ushirikina wa dini wanampa sifa Mungu"-hivyo ndivyo makafiri wanazingatia maombi yaliyojibiwa.

Hata hivyo,kuna chanzo kimoja cha uthibitisho ambao HAUPINGIKI! Chanzo hiki cha uthibitisho anaweza kuchunguza na macho yake na kuonyesha kuwa ni uongo-ikiwa Mungu hayupo!

Biblia yenyewe inaonyesha kuwa haina dosari,ufunuo utukufu wa ukweli uliofunuliwa na Mwumbaji na Mtawala Mtukufu wa ulimwengu.Katika Biblia,MTU AMETAJWA.Anadai kuwa ni Mungu.Anaongea katika nafsi ya kwanza akisema kuwa anaweza kutengeneza au kuharibu mataifa,kwamba anaweza kutekeleza hukumu zake-uamuze wake-kwa miaka elfu ya wakati,anadai kwamba anaweza anaweza kutabiri mambo yasiyo na dosari yajayo ya miji na utawala,lakini HAKUNA MTU awezaye kufanya hivyo.

NI NANI HUYU ANATAJWA AKISEMA:

Mimi ni Mungu,wala hapana aliye kama Mimi,nitangazaye mwisho tangu mwanzo,na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado;nikisema,Shauri langu litasimama,nami nitatenda mapenzi yangu yote,...;naam nimenena,nami nitatekeleza,nimekusudia nami natafanya.(Isaya 46:9-11)

Haya ni maneno ya anayedai kuwa Mungu-akidai ya kwamba anajua yajayo na tena ANAJUA KWA SABABU NI YEYE ANAAMUA – ANA NGUVU ZA KUFANYA MAPENZI YAKE!

#### KUWADHIHAKI Wasioamini

Wasioamini,kwa hakika,wanasema kwamba Biblia SIYO Neno linaloongozwa na Mungu,lakini ni maandiko tu ya kidini yasiyo na maana ya mataifa ya Wayahudi wa kale,ambao walijipapasa katika giza ya ujinga na ushirikina,wakijaribu kuendeleza dhana ya waliyofikiria Mungu alisema kuwa yupo. Lakini,je,ni hivyo? NI NANI HUYU anadai kutabiri yajayo? Je,ni mtu tu mjinga,mshirikina,angalau wema,Myahudi wa kale asiye na nguvu ya kutengeneza vizuri dhana yake iliyobuniwa ya Mungu,ambaye aliandika changamoto ya mashambulizi kwa wasioamini?

Hapa katika Biblia ni Mtu anaongea ambaye hawezi kubahatisha tu kile kitakachofanyika,lakini Yule anayedai KUJUA kwa sababu ANAJUA YAJAYO.Kwa sababu Huyu anaongea kupitia kwa maandiko,hapa ni thibitisho ambayo wasioamini wanahitaji.Ikiwa Mungu anaweza KUTEKELEZA Neno lake,ikiwa anaweza KUITIMILIZA unabii alionena kitambo katika karne ya 21-BASI WASIOAMINI WATATHIBITISHA MUNGU NDIYE MWANDISHI YA NENO LAKE ANAVYODAI KUWA.

Lakini kama matukio ni KINYUME cha maelezo ya Unabii wa Biblia-kinyume cha maadai ya huyu "Mungu"-basi wasioamini wamepata thibitisho kwamba Biblia haiaminiki-kwamba hatuwezi kuitegemea Biblia.

UNABII NI MIMOJA YA THIBITISHO AMBAPO MAANDIKO YANASIMAMA AMA YANAANGUKA! Hata "Mungu wa Biblia" anatambua ukweli huu.Anasema hapa hivi:

"Haya,leteni maneno yenu ,asema BWANA;toeni HOJA zenu zenye nguvu,asema mfalme wa Yakobo.Wayatangaze na kutujulisha yatakayokuwa;watuonyeshe mambo ya zamani,ni mambo gani,tukapate kuyatia moyoni,tukajue mwisho wake;au wamdhahirishie yatakayotokea baadaye.(Isaya 41:21-22)

Ndio,watu wadogo wanaokufa,ONYESHENI THIBITISHO WENU! Je, Siye mtu yejote lakini Mungu anatabiri? Biblia inaweza kuwa kazi ya binadamu pekee,bila msukumo wa Mungu,na ujazwe na unabii uliotimilika ambao uliandikwa karne zilizopita,ndio,maelfu ya miaka iliyopita mapema?

Mungu anasema,vile ilivyokuwa, "Kwa WEWE si kitu kabisa.Fikeni! Wacha tusikie unabii wenu ili kwamba tuone kama yatatimika au la.Tabiri yatakayofanyika siku zijazo,na wacha tutazame tuone kama unaweza kutabiri.Je,unayo uwezo wa kuutimiliza vile niufanyakyo?Je,ninyi ni mungu? Unatawala ulimwengu,ninyi amba mna shaka? Je,unaweza kutengeneza na kubomoa mataifa? Unaweza kutamka hukumu au amri kwa taifa,NA KUITEKELEZA?

Hiyo ndiyo dhihaka ya Mungu wa Biblia kwa WALIO NA SHAKA.

#### **Ukweli Umeonyeshwa kwa Urahisi**

Ndiyo,unabii unaotimilika ni THIBITISHO la utukufu wa ufunuo! Ikiwa mtu,kwa Biblia mzima,anaongea na kudai kuwa ni Mungu,anaweza kufanya unabii na kusema kitakachotokea katika siku zijazo kwa miji,mataifa,utawala wa ulimwengu huu wetu;basi IKIFANYIKA KWA NJIA YOYOTE,bila kukosa,hakuna akili timamu inayoweza kukataa kwamba MUNGU alisema hayo.

Ikiwa unabii wa Biblia ni wa hakika,basi UKWELI UNAWEZA KUONYESHA KWA URAHISI-amba wasioamini na wakanaji wameogopa.Anataka kubaki kwa ujinga wake.Anajivunia kuwa mkanaji ama aliye na shaka.Anajivunia ujinga!Lakini huwezi kujimudu kuwa katika ujinga-maisha yako ni ya thamani sana.Kuna vitu vingi sana vinatakikana!

Sasa tuko tayari kusoma Somo muhimu sana katika kozi mzima.

Je,umeweka Biblia mbele yako? Je,unayo makaratasi,kalamu hata ya risasi,ili UANDIKE uliyosoma upate kukumbuka ulichosoma? Kama sivyo,enda uchukue Biblia yako na unachohitaji.

Sasa na Bibli yako,karatasi yako na kamusi nzuri,na kitabu chochote unaweza kuhitaji (Kilichotajwa katika Somo la 4),hapa ndipo MBINU ya kusoma:Andika vizuri kwenye daftari lako maelezo "Somo la 10" na upige mstari.Chini yake,ndika kichwa cha swali la sehemu ya kwanza.Alifu,chini yake,ndika nambari ya kila swali,NA UANDIKE JAWABU PAMOJA NA MAANDIKO YANAYOTOA MAJIBU.Kama MFANO WA swali lako la kwanza,hili ndilo utakaloandika katika daftari lako:

1.Warumi 3:16—"Uharibifu na mashaka yamo njiani mwao."

Pia andika fikra au maelezo ungetaka kukumbuka.Ukimaliza swali hili na umelisoma na kuhakikisha umelielewa,alifu usome kifaa kinachofuata.Andika chini majibu yote yanayofuata ili uyatunze katika mawazo yako na KUYAPITIA BAADAYE.Maandiko unayopewa katika Kozi hii yatajenga muundo wa mfumo wa maarifa YOTE ya Biblia.

Kumbuka,unatakikana kutumia WAKATI ukisoma BIBLIA YAKO na Kozi hii ya Biblia.Hii itakusaidia kujua sana.

#### **SOMO LA 10**

#### **Thibitisho la Kwanza:Unabii wa Zamani Umetimilika**

Kuna unabii mwangi wa zamani katika Biblia amba ulitimilika.

Watu wengi wanaozoea Biblia wanatambua kwamba Wakristo wanafundisha kuwa Yesu alitababiriwa katika unabii wa Waerania amba umo ndani ya Agano la Kale.Na kwamba Wakristo wanadai Yesu alitimilisha unabii huo katika Agano Jipy.

Lakini wengi hawagundai kwamba unabii mwangi wa zamani ulitimilika katika historia ya kawaida.Hili ni tukio la sehemu ya Danieli 11 kutoka kwa Herbert W.Armstrong:

Nami sasa nitakuonyesha yaliyo kweli.Tazama,watasimama wafalme watatu katika Uajemi;naye mfalme wa nne atakuwa tajiri kuliko hao wote;naye atakapopata nguvu kwa utajiri wake,atawachochea wote juu ya ufalme wa Uyunani.Na mfalme hodari atasimama,atakayewatawala kwa mamlaka kubwa,na kutenda appendavyo.(Danieli 11:2-3)

Hakika kulikuwako wafalme 12 katika Utawala wa Uajemi,lakini wa nne walioanza waliofuata Koreshi walikuwa wa muhimu sana kwa kusudi la unabii huu.Walikuwa Ahasuero,Artashasta,Dario na Sasa. Alikuwa wa mwisho au Sasa,ambaye alikuwa tajiri sana kwa wote na akaanza vita na Ugiriki.

Alifu mfalme Filipo wa Makedonia akapanga vita kuu kushinda Utawala wa Uajemi,na wanajeshi wengi wa Wagiriki.Alikufa kabla hajamaliza mipango yake.Lakini mwanawewe Aleksanda Mkuu ,aliendeleza mpango wake na akavamia Uajemi.Alikutana na wanajeshi wa Uajemi katika vita vya Isusi,333 K.K.(Danieli

8:2,5-6).Halafu akapenya ndani ya Misri,na baadaye mashindano ya kuponda ya Utawala wa Uajemi katika vita vya Arbellia,331 K.K.baadaye Aleksanda alienda kwa ushindi kumaliza mpaka Hindi,akifagia kila mtu aliyejewa mbele yake.

Kumbuka mstari wa 4 ya unabii: "Naye atakaposimama,ufalme wake utavunjika,na kugawanyika katika pepo nne za mbinguni;lakini haukuwa wa uzao wake,wala hautakuwa wa kama mamlaka yake ambayo alitawala kwayo;kwa maana ufalme wake utang'olewa,hata kwa ajili ya wengine zaidi ya hao."

Ni ajabu ilioje-ni kwa usahihi unabii huu ultimilika.Tunanukuu kutoka kwa historia yenyenye mamlaka ya Kiingereza zilizochapishwa katika karne ya mwisho,Mwongozo wa Historia ya Kale ( Mfululizo wa Wanafunzi) na Rawlinson: " Akakatwa kwa ghafula katika nguvu za ujana[Miaka 33 ya umri wake,Juni 323K.K],yeye [Aleksanda] hakuacha mrithi,ya utawala wake au miradi yake" (Uk.237).Utawala uliachwa bila kiongozi na katika machafuko,lakini kutoka kwa huu ufalmulichipuka,mnamo mwaka wa 301 K.K.,zamu nne,vile ultabiriwa,kwa sababu ya mgawanyiko wa utawala katika zamu nne na jenerali ya Aleksanda.Walikuwa ni:

1.Ptolemy (Soter),aliyetawala Misri,sehemu ya Siria na Uyahudi.

2.Seleucus (Nicator),aliyetawala Siria,Babeli na wilaya ya Mashariki ya Hindi.

3.Lysimachus,alitawala Asia Mdogo.

4.Cassander,alitawala Ugiriki na Makedonia.

Basi unabii wa mstari wa 4 ukatimilika ulivyoandika.

Sasa tazama kumbukumbu inayofuata.Kutoka hapa Unabii unatabiri shughuli za zamu mbili kati ya zamu hizo nne: Misri,inayoitwa "Mfalme wa Kusini," kwa sababu ni Kusini mwa Yerusalem;na ufalme wa Siria,mfalme wa Kaskazini,hapo Kaskazini mwa Uyahudi.Ni kwa sababu Nchi Mtakatifu ilipita nyuma na mbele kati ya zamu hizo mbili,na kwa sababu vita vyao tofauti sanasana vilikuwa vya kumiliki Uyahudi,kwa hivyo unabii umewahu. Hapa ni mstari wa 5:

"Na mfalme wa kusini atakuwa hodari;na mmoja wa wakuu wake atakuwa na mamlaka;mamlaka yake itakuwa mamlaka kubwa."

Katika historia,tunajifundisha kwamba Ptolemy 1,aliyeitwa Soter,alikuwa mwenye nguvu na uwezo aliyeendeleza Misri zaidi ya ndoto za Aleksanda.Mmoja ya wafalme wake au jenerali,Seleucus Nicator,pia akawa na nguvu na uwezo.Na katika 312 K.K.,akachukua nafasi ya Ptolemy aliyefungwa katika vita,akawa imara katika Siria,na kuchukua taji kama mfalme.

Mstari wa 6 unasema:

"Na baada ya miaka kadha wa kadha watashirikiana;kwa kuwa binti wa mfalme wa kusini atakuja kwa mfalme wa kaskazini ,ili kufanya mapatano naye (pembeni, "haki" au "masharti sawa" ama "umoja wa ndoa"):lakini hatakuwa na nguvu za mkono wake sikuzote;wala mfalme yule hatasimama,wala mkono wake;lakini yule binti atatolewa,na hao waliomleta,na yeze aliyemzaa,na yeze aliyemtia nguvu,zamani zile."

Ulitimilika kamili ilivyoandikwa!

Katika mwisho wa miaka 50,hili lilifanyika vile ulivyoelezwa!

Mtawala wa siria,mfalme wa kaskazini,wakati huu alikuwa Antioka 11,aliyeitwa Theos.Mke wake aliitwa Laodiki.Na historia ya kitambo ya Rawlinson,ukurasa 251, "Ushawishi wake-ilimhusisha katika vita na Ptolemy Philadelfas (mfalme wa kusini),252 K.K. na ndoa kati ya Antiokas na Bernice,binti wa Ptolemy."

Unabii unasema, "alimzaa" na atasimama. Na pia hatakuwa na nguvu za mkono,na hata mfalme wa kaskazini aliyeoa,hatasimama.Zote tatu zinafika mwisho.Kumbuka vile unabii huu unatimilika.

Historia ya Rawlinson ukurasa wa 251 na 252 inasema: "Wakati wa kifo cha Philadelfas (aliyemzaa),K.K.247,Antiokas alikana Bernice na akarudisha mke wake wa kwanza,Laodiki,ambaye,walakini,alitia shaka kwa msimamo wake,alimwua ili asipate kitie cha enzi kwa mtoto wake Seleus (11) K.K. 246....Bernice aliwekwa kwa kifo na Laodiki."

Hakuna mahali popote katika Biblia pamekuwa na unabii unaotupatia kila kitu kuhusu historia yajayo.Na kusoma historia ya kale ya falme hizi ni kuona vile inavyofunuliwa machoni pako,hatua kwa hatua,unabii huu wa kiajabu.Hakuna shaka ya ya matumizi yake sahihi!"

## Nchi Takatifu Imeshikana Mikono

Wacha tutazame mstari wa 7:

"Lakini katika chipukizi la mizizi yake atasimama mmoja mahali pake atakayeliendesa jeshi la askari,naye ataingia katika ngome ya mfalme wa kaskazini,na kuwatenda mambo,na kuwashinda."

"Kutoka kwa tawi," au "chipukizi," ya mizizi yake.Wazazi wake ndio mizizi yake.Kwa hivyo,huyu lazima ni ndugu yake,ambaye atachukua kitu cha enzi cha mfalme wa kusini na kutimiliza unabii huu.Sasa sikiliza utimilifu huu kamili,unaotajwa moja kwa moja kutoka ukurasa wa kazi ya Rawlinson (uk 252):

"Ptolemy Euergetes (wa III,kijana wa kwanza wa Philadelfas (uk.272) na kwa hivyo ndugu ya Bernice,tawi ya mizizi yake) alivamia Siria,K.K.245, kulipiza kisasi kifo cha dadake aliyeuawa,Bernice....Katika vita vilivyofuata,alibeba kila kitu alichopata."

Mstari wa nane wa Danieli 11 unasema kwamba mfalme wa kusini atabeba mateka na vyombo vyya fedha na dhahabu mpaka Misri,na akaendelea kutawala miaka mingi kuliko mfalme wa kaskazini,ambaye kwa wakati huo alikuwa Seleucus II, na mstari wa 9 unasema atarudi mpaka Misri.Kama vile mstari wa 7 unasema "ataingia katika ngome ya mfalme wa kusini," Ptolemy III alikamata ngome ya Siria,Seleucia,bandari ya Antiokia jiji kuu la ufalme!Alafu akabebe mpaka Misri ngawira kubwa na 2,500 sanamu zilizochongwa na vyombo vyya sanamu ambavyo katika mwaka wa 526 K.K.Cambyses alibeba kutoka Misri.Aliendelea kutawala mpaka mwaka wa 222 K.K.,wakati mfalme wa kaskazini,Seleucus II,alikufa mnamo mwaka wa 226 K.K.

Wakati alikufa,vijana wake wawili walichukua ufalme wa kaskazini;wa kwanza Seleucus III,226-223 K.K.,ambaye alitawala miaka mitatu pekee yake,na nduguye Antiokas III,aliyeitwa "Mkuu," 223-187 K.K.Wote hawa walisanya jeshi kubwa kupigana na Misri kulipisha kizazi baba yao,na kurudisha bandari yao na ngome yao,Seleucia.

Na huu ulitabiriwa vyema katika mstari wa 10:

"Na wanawe watafanya vita,na kukusanya mkutano wa majeshi makuu;watakaokuja na kufurika na

kupita katikati;nao watarudi na kufanya vita pengine mpaka ngome yake."

"Na," inaendelea mstari wa 11,

"Na mfalme wa kusini ataingiliwa na ghadhabu,naye atatoka na kupigana,yaani na mfalme wa kaskazini;naye atapanga jeshi kubwa;na jeshi hilo litawekwa mkononi mwake."

Katika kutimilika kwa sehemu ya mwisho ya mstari wa 10,Antioka Mkuu,baada ya miaka 27,alirudisha ngome yake,Seleucia,na pia akashinda wilaya ya Siria,hadi Gaza mpaka Uyahudi.Lakini mfalme mdogo wa Misri,ambaye alikuwa Ptolemy IV (Philopater),alihamshwa na pamoja na wanajeshi 20,000 alisababisha ushindi mkali kwa Antiokas Mkuu;na kuutimiliza mstari wa 12,aliwauwa maelfu na pia akaongeza Uyahudi na Misri.Lakini hakuongezewa nguvu,kwa sababu alifanya pupa na haraka ya kufanya amani na Antiokas,na akarudi kwenye maangamizi,alipotupa matunda ya ushindi.Mstari wa 12 inasema, "Atakapokwisha kuchukua lile jeshi,moyo wake utatukuzwa;naye atawaangusha makumi elfu;lakini hataongezewa nguvu."

Na mstari wa 13 unaendelea,

"Kwa maana mfalme wa kaskazini atarudi,naye atapanga jeshi kubwa kuliko lile la kwanza;naye hakika atakuja mwisho wa zamani zile,yaani,baada ya miaka kadha,pamoja na jeshi kubwa na mali nyangi."

Ilikuwa baada "miaka kadha," ya 12 baadaye,205 K.K.,ambayo Ptolemy Philopator alikuwa,na kuwachilia kitu cha enzi kwa mtoto mchanga,Ptolemy Ehiphanes.Alafu Antiokas alisanya jeshi kuu,na kushinda ushindi mkuu. Baadaye alitengeneza mkataba uliomshirikisha Filipo wa Makedonia na yeze na wengine dhidi ya Misri,na wakawapiga mireka Phoenicia na Siria kusini kutoka kwa mfalme wa kusini.Katika haya walisaidiwa na wayahudi wengine. Yosephus,historia ya Wayahudi inasema Wayahudi wengi walisaidia Antiokas.Lakini kumbuka vile Mungu Mwenyezi alitabiri kisa hiki,miaka mingi kabla hakijafanyika!-

"Na zamani zile watu wengi watasimama ili kumpinga mfalme wa kusini;pia wenye jeuri mionganii mwa watu wako watajiinua ili kuyathibitisha maono;lakini wataanguka." (Mstari 14)

### Soma Katika Biblia Yako!

Kuokoa nafasi,msomaji anaulizwa kutoka hapa asome kila mstari kutoka kwa Biblia yake,ili atuokoe uchapishaji wa unabii mzima hapa.Tunawapatia uhakika pekee katika historia.

Mstari wa 15-16—"Nchi ya uzuri," hakika inamaanisha Uyahudi,Nchi Takatifu.Antiokas Mkuu alichukua Sidoni kutoka Misri,akaharibu maslahi ya Misri katika Uyahudi kwenye Vita vya Mlima Panium,198 K.K.,na baadaye Antiokas akachukua milki ya Uyahudi.

Mstari 17—"wenye maadili"...Katika 198 K.K.,Antiokas alipanga ndoa kati ya binti yake,Cleopatra (siye Cleopatra wa 31 K.K. wa Misri) na Ptolemy Epiphanes mdogo,mfalme wa kusini,aliyetumai kuchukua milki yote ya Misri;lakini mpango huu ukaanguka.

Rawlinson alisema kwa ukarasa wa 254, "Koli – Siria na Palestina waliahidiwa kama mahari,lakini hazikutolewa." Cleopatra hakusimama kwa upande wa Antiokas,kwa sababu ilikuwa mbinu ya kupata umiliki wa Misri.

Mstari wa 18-na Antiokas aligeuza mawazo yake kwa njia nyingine na kujaribu kushinda,197 mpaka 196 K.K.,visiwa na puan za Asia Ndogo.Lakini Jenerali wa Rumi,Lucius Cornelius Scipio Asiaticus,alimshinda zaidi katika vita vya Magnesia,190 K.K.

Mstari wa 19-Antiokas tena akageuza mawazo yake kwa ngome ya nchi yake,katika Kusini na Magharibi.Lakini akijaribu kuandikisha mali yake aliyefuja kwa uporaji wa Hekalu la Mashariki la Belusi,katika Elymaisi,aliuawa mnamo mwaka wa 187 K.K. (Armstrong H.W.Mashariki ya Kati Katika Unabii.Kanisa la Mungu Ulimwenguni Pote-WCG,1972)

Kitabu cha Danieli kiliandikwa mwaka wa 540 K.K. ama zaidi.Hata hivyo,kumbuka unabii mwiingi katika mlango wa 11 za kitabu hiki ulitimika kihistoria.Watu wengi,hata wenye hawana haja na historia wamesikia Aleksanda Mkuu na Cleopatra-na walivyofanya vilitabiriwa karne nyingi mapema katika Biblia.

Kwa hakika,kuna wakanaji na wenye shaka ambaa wanadai kwamba kitabu cha Danieli hakikuandikwa kabla ya mambo haya kuyatokeaa.Wengine hawatakubali ukweli na kuamini kwamba mtu yeote ama hata Mungu anaweza kutabiri mambo yajayo.

Tazama pia yafuatayo kutoka kwa Muinjilisti wa kanisa la Mungu Leroy Neff mahali alitaja kuhusu utimizaji ikiwa ni pamoa na mengi kuhusu Aleksanda Mkuu:

### Koreshi,Mtawala wa Uajemi

Mfano wa kwanza ni wa Koreshi Muajemi,mtawala wa kwanza wa Himaya ya Uajemi,aliyeishi katika karne ya sita K.K.Hadithi za kuzaliwa kwake Koreshi na ujana wake vile zimerekodiwa katika historia za wakati,zina maarufu sana hadi zinaonekana kama kwamba ni hadithi za watoto.Herodotus ambaye ni mwanahistoria wa karne ya tano K.K.,akieleza moja ya hadithi hizo hapa anatoa kwa muhtasari.

Astyages,mwana wa Cyakseres,mfalme wa Mmedi alikuwa na binti aliyeitwa Mandane.Aliogopa kwa sababu aliota kuwa binti yake atazaa mtoto atakayetawala kwa nafasi yake,na sio ufalme wake pekee lakini Asia mzima.Alikuwa anataka kuzuia hii kwa njia yoyote.

Wakati Mundane alipata mtoto wake wa kwanza,kijana,Astyages aliagiza mmoja kati ya watumishi wake aliyeamini sana,Harpagus,apate kumwua mtoto huyo.Harpagus kwa vile hakutaka kufanya tendo hilo la kutisha,alikabidhi jukumu hilo kwa Mitrirates,aliyekuwa mchungaji wa ng'ombe.Mitrirates,alipopata kwamba mimba ya mke wake ilitoka,alichukua na kulea kijana wa Mundane kama mtoto wake.Wakati kijana alifika miaka 10 alipata kutambulika.

Babu yake,Astyages,mfalme sasa alimkubali na baadaye huyu kijana,Koreshi,alipanda kwenye kiti cha enzi mwaka wa 558 K.K.Mnamo mwaka wa 559 K.K.Koreshi alikuwa mfalme wa Media,na mnamo 548 K.K. alitawala Uajemi mzima;Alishinda Babeli mwaka wa 539 K.K. na himaya ya Uajemi ilifuata utawala wa Babeli.

Hadithi hii ingekuwa na maarufu pekee yake lakini utabiri huu unapatikana katika unabii wa Biblia.Utaupata utabiri huu katika mistari ya mwisho wa Isaya 44 na sehemu ya kwanza ya Isaya 45.

"nimwambiyaye Koreshi,Mchungaji wangu,naye atayatenda mapenzi yangu;hata ataunena Yerusalem, Utajengwa;na hilo hekalu,Msingi wako utawekwa."(Isaya 44:28)

Isaya alitoa unabii huu karne mbili kabla Koreshi hajatangaza kuhusu kujenga tena Hekalu ya Yerusalem!

"Koreshi,mfalme wa Uajemi asema hivi;BWANA,Mungu wa mbinguni amenipa falme zote za dunia;naye ameniagiza nimjengee nyumba katika Yerusalem,ulioko Yuda." (Ezra 1:2)

Mungu alimtaja Koreshi kabla hajazaliwa na pia aliona kwamba babu yake hakumwua! Aliweza kuona vile Koreshi alitangaza kujenga upya Hekalu,vile Mungu alisema atafanya! Lakini kuna mengi.

#### **Milango Miwili Inayoachana**

"Haya ndio BWANA amwambiyayo Koreshi,masihi wake,ambaye nimemshika mkono wake wa kuume,ili kuutisha mataifa mbele yake,nami nitalegeza viuno vya wafalme;ili kufungua milango mbele yake,hata malango hayatafungwa." (Isaya 45:1)

Isaya alitabiri kwamba Mungu atawezesha Koreshi kushinda falme nyingi ambazo baadaye zikawa chini ya utawala wake.Pia "milango miwili inayoachana" haitafungwa.Hii inaashiria njia ya ajabu Koreshi aliteka jiji (na hata himaya) ya Babeli.

Jiji kuu la Babeli na kuta lake refu na kubwa,lilionekana lisiloshindika kutoka nje.Wakati wanajeshi wa Koreshi walipiga kambi wakizingira jiji,wa Babeli walicheka! Wangeishi mazingwa ya miaka!

Bila kujulikana kwa watu wa Babeli,hata hivyo,watu wa Koreshi wangeweza kuugeuza mto Frati,ambao mara nyingi ultiririka kuitia malango makubwa kwenda ndani ya jiji.Koreshi alipata ujasusi aliyeingia jijini,ambaye alifungua milango ya ndani kwenye mto.Na kwa kiwango cha chini cha mto,wanajeshi waliweza kuvamia jiji kwenye njia ya mto na kuitia kwa milango hii,akiwachukua Wababeli kwa mshangao mkubwa.Sehemu ya ajabu ya Utimizaji wa unabii kuhusu "milango miwili" umelezwa katika Danieli 5,mengine yanapatikana katika historia za kawaida.

#### **Ushindi wa Aleksanda**

Mhusika wa pili wa unabii tutakaongalia ni Aleksanda wa Makedonia,pia anayejulikana kama Aleksanda Mkuu.Alikuwa mfalme wa kwanza wa utawala wa Ugiriki-Makedonia.Wakati wa kifo cha babake Filipo katika mwaka wa 336 K.K.,alipanda kwenye kitu cha enzi cha Ugiriki akiwa miaka 20 peke yake. Miaka miwili baadaye,aliingia Asia na kikosi cha miguu 30,000 na cha farasi 5,000.Aliweka kwa ndege wanajeshi bora sana wa Uajemi katika vita vya Granikas na baadaye mnamo Oktoba 1,331 K.K.,alimenyana na Dario III,mfalme wa Uajemi ambaye alikuwa na wanajeshi mara 10 kuzidi yake.Vita hivi vya Isa vilimshindia sana ushindi wa ajabu.Aleksanda baadaye alishinda ushindi wa kuthibitisha juu ya Abela mnamo Oktoba 1,331 K.K.,hata hivyo,Dario III alimzuia zaidi ya wanajeshi milioni moja.

Huyu bwana mdogo aliendelea kupanua himaya yake mpaka mto wa Inda.Alikuwa kwa homa akiwa na miaka 34,baada ya utawala wa miaka 13 peke yake.Unabii kuhusu mtu huyu unapatikana katika Danieli 8 na 11.Sehemu ya unabii huu unasema:"Nami nilipokuwa nikifikiri,tazama beberu akatoka upande wa magharibi,juu ya uso wa dunia nzima,bila kuigusa nchi;na beberu yule alikuwa na pembe mashuhuri kati ya macho yake.Naye akamwendea huyo kondoo mume mwenye pembe mbili,niliyemwona akisimama karibu na mto,akimshambulia kwa ghadhabu za nguvu zake." (Danieli 8:5-6)

"Pembe"hiyo inaashiria Aleksanda(mfalme wa kwanza wa Uyunani,mstari wa 21) ambaye alishinda "kondoo"(mfalme wa Uajemi,mstari wa 20).Aleksanda pia ameonyeshwa katika Danieli 11:3-4.

Unabii huu ulipewa Danieli katika karne ya sita K.K. lakini utimizaji wake wa Aleksanda haukufanya mpaka karibu karne mbili baadaye,mnamo karne wanne K.K.

#### **Wayahudi Walindwa**

Upande wa unabii huu wa kusisimua unahuji jiji la Yerusalem na Wayahudi waliomo ndani yake.Wakati Aleksanda alikuwa akiendesha sehemu ya kusini,baada ya kushinda Siria,alipitia Yerusalem,akiendelea kwenye pwani ya bahari kuelekea Gaza,aliyechukua katika mwanzo wa mwaka wa 332 K.K.Baadaye alienda na wanajeshi wake hadi Yerusalem.

Alikuwa ameamwandikia Yadua,kiongozi wa Wayahudi na kuhani mkuu,akihitaji riziki nyingine.Yadua alimjibu kwamba alikuwa amekula kiapo kwa mfalme Dario wa Uajemi ambacho hawezi kukiuka wakati Dario alikuwa akiishi.Neno hili lilimkasirisha Aleksanda:

"Basi Aleksanda baada ya kuchukua Gaza,alienda upesi Yerusalem,na Yadua kuhani mkuu aliposikia haya,alijawa na huzuni na aliogopa vile atakutana na Wamakedonia,kwa sababu mfalme alikashirika na kutotii kwake"(Josephus,Ant.,Book XI,Chapter VIII,section 4).

Yadua aliwahimiza watu waombe na kutoa dhabihu kwa Mungu,alafu Mungu akamwambia katika ndoto jinsi ya kupokea Aleksanda na wanajeshi wake.Hapa panaeleza vile mkutano wa muda huo ulifanyika.

"Aleksanda,alipoona umati kwa mbali katika kanzu nyeupe,wakati makuhani walismama wakivaa kitani safi na kuhani mkuu akivaa nguo ya zambarau na nyekundu,na kilemba kichwani mwake,ikiwa na bamba ya dhahabu kwake,jina la Mungu limeandikwa juu ,alisogea peke yake na kumsujudu jina hilo,na kumpigia saluti kuhani mkuu."

Aleksanda baadaye akasema:

"Nilimwona huyu mtu katika ndoto,akiwa na asili hii,nikiwa Diosi wa Makedonia,ambaye nilipokuwa nikishauriana naye jinsi ya kuchukua mamlaka ya Asia alinihimiza kwamba nisichelewe....Na wakati alionyeshwa kitabu cha Danieli,ambamo Danieli anasema kwamba mmoja wa Wagiriki angeharibu himaya ya Wajemi,aliona kwamba ni yeye alitarajiwa kufanya hivyo.(Hapo sehemu ya 5)

Kwa sababu ya matukio haya,Aleksanda alifanya huruma sana kwa Wayahudi.Hadithi hii ya kusimua inaleta maelezo zaidi jinsi Mungu anatimiza unabii wa Biblia,wakati mwininge kwa njia za ajabu.

#### **Machukizo Ndani ya Hekalu la Mungu**

Tukio la mwisho tutakaloangalia linahusiana na Antiokas Epiphanes,ambaye alikuwa mfalme wa Siria katika karne ya pili K.K.

Baada ya kifo cha Aleksanda himaya yake iligawanywa katika falme nne (Danieli 7:6,8:8,22,11:4).Mmoja kati ya falme hizi ni Siria.Danieli anasema hivi kuhusu Antiokas:

"Na katika moja ya pembe hizo ilitokea pembe ndogo,iliyokua sana upande wa kusini,na upande wa magharibi,na upande wa nchi wa uzuri.Nayo ikakua,kiasi cha kuifikilia jeshi la mbinguni;ikaangusha chini baadhi ya jeshi lile,na nyota ikazikanya.Naam,ikajitukuza hata juu ya aliye mkuu wa jeshi hilo,ikamwondolea sadaka ya kuteketezwa ya daima,na mahali pa patakatifu pake pakaangushwa chini.Na jeshi likatolewa kwake pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya daima,kwa sababu ya makosa;nayo ikaangusha kweli hata chini;ikatenda ilivyopenda,na kufanikiwa." (Danieli 8:9-11)

Unabii huu ultimilika kwa njia ya kutisha.Antiokas alichukua Yerusalem na Hekalu.Alikomesha sadaka ya kila siku na kulazimisha dini ya pagani kwa Wayahudi.Hapa ni muhtasari wa maelezo ya kutisha:

"Maadhimisho ya Sabato,tohara na kutokula vyakula chafu yalipigwa marufuku chini ya adhabu ya kifo.Kina mama waliopatikana wakitahiri watoto wao walisubiwa na watoto wao kuning'iniwa kwenye shingo yao.Sadaka za kila siku zilikomeshwa.Madhabahu ya Zeusi wa Olimpia yalijengwa juu ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na dhabihu ilitolewa juu yake.Patakatifu sana na samani zake zilinyunyiziwa mchuzi wa nyama ya nguruwe.Sehemu za hekalu zilitiwa unajisi na karamu zisizo na heshima.(Historia ya kale ya mwangaza wa Biblia,Miller,uk 214)

Wakati huu kwa nadra sana ,kama ikiwa,unaweza kulinganishwa katika historia ya Israeli na Yuda.Sio kwamba watu walichinjwa na kukaangwa katika sufuria kubwa pekee yake lakini pia Antiokas mwenyewe alilingia patakatifu pa patakatifu katika Hekalu la Mungu na kuchukua vyombo katika Hekalu.Alisimamisha "Madhabahu ya Ugiriki kwenye eneo la madhabahu ya zamani mnamo 25 Desemba,167" (Kamusi Mpya ya Biblia,Jarida "Antiokas").

Hatimaye Yuda Makabayo,ndugu zake na Wayahudi waliweza kuchukua tena

Yerusalemu miaka mitatu baadaye,wakasafisha patakatifu (Hekalu) na wakarudisha ibada ya Mungu.

Inafaa tukumbuke hapa kwamba,basi,kuwa unabii wa Danieli 8:9-12 ni mara mbili.Antiokas alitimiza unabii huu kwa ajili ya wakati huo lakini bado unangoja utimizaji wa kutisha sana katika nyakati za mwisho!

#### **Unabii wa Leo**

Mifano hii mitatu inaonyesha kwamba Mungu anajua mwisho kutoka mwanzo na kutabiri yajayo,pia anaona kwamba unabii wote umetimilika.

Hakika vitabu vingi vingeandikwa-vimeandikwa-kuleta kinaganaga cha historia.Kuna baadhi ya unabii uliotimilika wa Kristo pekee,mwingine kuhusu Yohana Mbatisaji,Yuda Iskariote na wengine.Kuanguka kwa Israeli na Yuda pia kulitabiriwa kwa undani zaidi na Isaya,Yeremia na wengine.Utimizaji wa ahadi ya kimwili kwa Ibrahimu ni suala la rekodi.

Marejesho ya Wayahudi kwao Uyahudi katika karne sita K.K.,kujengwa upya kwa Hekalu na kuanguka kwa Yerusalemu katika mwaka wa 70 B.K ni unabii mkuu ambao umetimilika.Kuinuka na kuanguka kwa Babeli pia ni unabii uliotimilika.

Kuanguka kwa mzao wa kisasa wa Israeli (hususan Uingereza na Marekani) bado kuko njiani.Hii ilitabiriwa kitambo wakati wa Musa (Walawi 26 na KumbuKumbu 28).Kuanguka huku kutasababisha wakati wa taabu ya Yakobo au dhiki kuu.Baada ya dhiki hii,ishara zisizo za kawaida za mbinguni zitatangaza kurudi kwake Yesu.Baada ya ishara hizi "Siku ya Mungu" itaanza inayokaribisha kurudi kwake Yesu Kristo kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

Unabii unaonyesha kwamba Mungu atatengeneza njia ya kuepuka hofu hizi kwa watumishi wake waaminifu ambao "wamestahili" (Luka 21:36).

Tunatakikana tufanye biashara ya Baba yetu,tukifanya kazi aliyetuamuru tufanye,tukisafisha maisha yetu ili pamoja na wengine ambao wamehitimu,tuwe "kanisa tukufu lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo" (Waefeso 5:27).

Tukifanya hivyo,tutaepuka matukio ya kusikitisha na kusimama mbele ya Mwana wa Adamu! (Unabii uliotimilika,Changamoto wa

Mungu kwa wasioamini.Gazeti la Habari Njema,Desemba 1980)

#### **Thibitisho la Pili:Ugomvi Ulitabiriwa**

Jambo moja lasimama kama SABABU kubwa ambayo inasababisha wengi kutia shaka kwenye unabii wa Biblia-Ni ASILI na MTAZAMO wa mwanadamu ya kuasi.

Unabii unaonekana jambo ambalo silo la asili kwa watu wengi-jambo ambalo haliwezi kutokea-kwa sababu unaonyesha Mungu ambaye anaweza KUKASIRIKA na dhambi za ulimwengu-Mungu ambaye anadai kujua zaidi ya vile TUNAPASWA kuishi.Unabii unadhihirisha Mungu ambaye anakosoa ulimwengu kwa sababu umeptoea kwa kuweka serikali yake na kuteua SHERIA ZAKE AMBAZO NI KINYUME NA SHERIA YA MUNGU NA SERIKALI YAKE.

Bila shaka ukweli wa kwanza ambao unatakikana tuangalie-ikiwa tunaenda kuelewa unabii na ASILI ya Mungu-unahusiana na ASILI YA MWANADAMU mwenyewe.

Hii ndiyo SABABU YA KIMSINGI YA UNABII!

1.Warumi 3:16,kama vile maeleo mengine ya maandiko,NI UNABII.Inasema nini?

Taja MATOKEO ya MAISHA YA WANADAMU WANAVYOISHI.Je,ulimwengu wote wanakabiliana na matokeo yasiyoepukika leo? (Tazama pia Somo la 1,Chanzo cha maovu ya ulimwengu,Unabii wa Biblia ,Januari-Mechi 2014,uk 17-19).

2.Linganisha mstari wa 15 na mistari mitano inayotangulia.

3.Biblia inasema nini kuhusu uwezekano wa BINADAMU kuunda AMANI YA ULIMWENGU bila Mungu kuingilia kati? Mstari wa 17.Tazama pia Yeremia 6:13-15 Warumi 3:13-18;Isaya 59:8;Ezekieli 7:25-26;na 1 Wathesalonike 5:2-6.

4.NANI anadai kwamba anaweza kuleta amani? Isaya 45:7

5.Je,haya maandiko yanadhihirisha moja kwa moja KWAMBA MUNGU PEKEE ANAWEZA KULETA AMANI ULIMWENGINI-ya kwamba walimwengu hawawezi kuunda amani bila yeze kuinglia kati?

6.Je,watu wanatambua maandiko haya kama unabii?Je,watu wanaamini maandiko haya kwamba yanamaanisha yaliyosemwa? Unajuaje kwamba watu hawaamini yanayosemwa katika maandiko haya?

Je,wanafikiria kwamba wanaweza kuleta amani ya ulimwengu wenyewe?

7.Je,maandiko haya yaliyoandikwa kuanzia miaka 1940 mpaka 2700 iliyopita,yanaonyesha kwamba anayedai kuwa mwandishi wa Biblia ALIJUA MATOKEO YA MWISHO ya njia za binadamu na desturi zake? Je,HALI YA ULIMWENGU WA LEO inadhibitisha kwamba anajua? (Kuangalia uchambuzi wa Biblia ya kila siku enda kwa [www.cogwriter.com/news](http://www.cogwriter.com/news).)  
Je,Mungu alitabiri kuanzia mwanzo wa historia ya binadamu,tunayoyaona yanatukia leo? Yuda 14-15.

Je, watu wengi wanakubaliana na utabiri wa Mungu?Je,unafikiri kwamba njia za ulimwengu zinaweza kuongoza kwa kuleta amani na utulivu mionganoni mwa mataifa?

Zingatia yafuatayo:

#### **Nyakati za Hatari**

Janga la ugaidi lilitabiriwa karne nyingi zilizopita katika kurasa za Biblia.

Yesu alitabiri kwamba hali katika nyakati za mwisho zitaangaza vurugu ya dunia kama nyakati wa Nuhu-ulimwengu mwovu na wa ufisadi ulioja na ghasia.(Luka 17:26,Mwanzo 6:5,11).

Mtume Paulo pia alionya, "siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari" (2 Timotheo 3:1).Maana ya unabii huu inaenda zaidi ya uhalifu muafaka.

"Ufue myororo;kwa maana nji hii  
imejaa hukumu za damu,nao mji  
umejaa udhalimu."(Ezekiel 7:23)

Unabii wa Biblia unaonyesha ulimwengu wa nyakati za mwisho zinazojaa uasi,uchokozni na chuki, ugomvi na migogoro ya kimataifa,zama ya kuenea,vurugu ya kiolela na mauaji yanayosukumwa na Ibilisi shetani,mwuaji wa awali (Yohana 8:44).Tunaishi katika siku hizo!

Binadamu,bila Mungu,hawawezi kudhibiti ugaidi.

Maadamu athari za Shetani zimebaki duniani,ugaidi na uhalifu zitaendelea kuenea,liche ya mwanadamu kujaribu kuziondoa.Nguvu itaendelea kutawala ulimwengu.Mwanadamu atajaribu kujibui uhalifu kwa uhalifu.Huu bado ni ulimwengu wa Shetani.(1 Wakorintho 4:4) (Stump K.Jinsi  
Ugaidi utakomeshwa! Gazeti la Habari Njema,Desemba 1985)

#### **UGAIDI Mbaya Zaidi Bado Unakuja!**

Wanaoua kwa bomu wanatishia ghasia katika Mashariki ya Kati.Na wataalamu sasa wanaonya kuhusu " ugaidi unaoungwa mkono na nchi." Yote haya yanaelekea wapi?

Makundi ya kigaidi wanaishi hata kama serikali wameweka vikwazo kama vile biashara inayoyumbayumba inaendelea hata kama kuna ugumu wa uchumi."Kuishi kwa bishara",makundi ya ugaidi wameiba benki,wamenyang'anya,wamepokonya,hata kuhusika katika mihadarati ama bidhaa za magendo. "Lakini mchango wao wa mitaa" haujafaulu kwa makundi mengine.Kwa hivyo,wameamua njia nyingine ya ukorofi zaidi ya kukuza bajeti yao:kutafuta wafadhili wenyewe nguvu ambao wanaweza kuwapatia mapumziko ya usalama,mazoezi,silaha na pesa.Wakati mwingine,wafadhili wamethibitishwa kuwa serikali ya kimataifa-ambao unaongoza kwenye kinachoitwa "ugaidi unaohifadhiwa na nchi."Wagaidi wamekuwa njia mataifa mengine ya nguvu wanaotamani kuepa kuenea kwa malalamiko ya umma,wanaweza kutumia kuadhibu maadui yao kwa bei rahisi.

Ufadhilli wa nchi umeonyesha uso mpya wa hatari ya ugaidi.Kwanza kiwango cha silaha zinazotumiwa zimeenda juu sana.Bomu ya mafuta chafu ya mfeleji zimechukua nafasi ya bomu ya moto ya magari.Mchanganyiko wa Motolov ziko nje;kombora ya guruneti zinazosukuma ziko.Lakini kiwango kikubwa cha pesa na silaha siyo mabadiliko ambayo yamekuja kwenye onyesho.Shabaha pia zimebadilika.(Taylor D.UGAIDI mbaya zaidi bado Unakuja! Ukweli Wazi,Mei 1984)

Kumbuka maandiko yafuatayo:

25 Nje upanga utawafifiliza.Na ndani ya vyumba.(Kumbukumbu 32:25)

12 Piga kelele,utoe sauti ya uchungu,Ee mwanadamu,kwa maana upanga u juu ya watu wangu,u juu ya wakuu wote wa Israeli;wametolewa wauawe na upanga pamoja na watu wangu,basi jipige pajani."(Ezekiel 21:12)

25 Bali mmebatilisha shauri langu,Wala hamkutaka maonyo yangu;26 Mimi nami nitacheka siku ya msiba wenu,Nitadhihaki hofu yenu

ifikapo;27 Hofu yenu ifikapo kama tufani,Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli,Dhiki na taabu zitakapowafikia.(Mithali 1:25-27)

5 Naam,wataogopa kilichoinuka.Na vitisho vitakuwapo njiani.(Mhubiri 12:5)

Wakati wanasiwa wengi,wanahabari,na viongozi wengi wanakataa kuamini Biblia,hakika ni kwamba wanaoamini Biblia kama sisi twagundua kwamba ugaidi umetabiriwa.

Kumbuka kwamba tumeona ongezeko katika 2015 na 2016.Ugaidi ulitabiriwa!

**MAELEZO:**Unabii huu ni changamoto kwa wakanaji na wasioamini!

MKANAJI NA ASIYEAMINI WANAWEZA KUDHIBITISHA KWAMBA MUNGU NI MWONGO KWA KUUNDA AMANI MIONGONI MWA WANADAMU BILA MUNGU KUINGIA KATI! Lakini ushuhuda wa historia ya mwanadamu unaonyesha kwamba katika miaka elfu mbili yote,mataifa ya ulimwengu hawajaweza kuupuzia unabii huu na kuunda amani ya kudumu! (Biblia inaonyesha wakati wa "mkataba" ambao utaleta amani kwa Mashariki ya Kati kwa miaka michache,lakini pia inasema kwamba mkataba huo utaleta mgawanyiko na vita tofauti vitakavyofuata baadaye katika Danieli 9:27;Danieli 11:31-44). Huu ni USHAHIDI HALISI UNAOONEKANA kwamba neno la Mungu linatimilika.Lakini ulimwengu unakataa KUGUNDUA USHAHIDI HUU! Bila shaka aliye na shaka anaweza kusema kwamba maandiko haya ni ujanja wa kukisia yanayopatikana katika historia ya kale! Historia ya binadamu inaonyesha lakini ni watu wangapi wanaamini?

Huu ni unabii ambao umesimama kwa karne nyingi,na unatimilika,NA HAKUNA MWANADAMU ANAYEWEZA KUUBADILISHA UNABII HUU! Mataifa wamemwaga damu galoni milioni ya watu,wakitumia milioni kadha ya pesa,wakiaribu wakati wao muhimu-wakifanya matendo ambayo Mungu alisema hayatawezekana.Na tutaona utimizaji wa unabii huu wakati Mungu ATAINGIA KATI katika shughuli za wanadamu KUZUIA MAANGAMIZO YA ULIMWENGU na kutuletea amani ya ulimwengu mwishowe!

Wakanaji na makafiri wanoishi sasa wataona siku hiyo! Mafundisho yote ya Biblia

yanasimama na kuanguka kwenye unabii huu wa kimsingi anathubutu mtu ye yote kuvunja!

### **Kanisa la Mungu Linatimiza Unabii**

Hata wakanaji wanaamini kwamba Biblia imeandikwa kwa umbo lake kamili katika karne 19 zilizopita.KWA HIVYO KILA NENO KATIKA BIBLIA LINALOHUSU KANISA AMBALO YESU ALISEMA ATALIJENGA HALIWEZI KUUNDWA KATIKA MIAKA MICACHE ILIYOPITA.Tuna nakala nyingi zinazothibitisha kwamba muswada wa Agano Jipy ya kisasa ni sawa vile ilivyokuwa karne 20 zilizopita.

Je,Yesu alisema nini litatokea kwa Kanisa Lake? Je,Kanisa lake litakuwa lenye nguvu, 'Mama' wa makanisa ambalo "binti" zake wanaoasi/Waprotestani watachipuka kutoka kwake? Je,Kanisa lake lingefika Babeli ya machafuko-katika madhehebu mengi yanayokinzana?

Ikiwa Yesu angeishi leo-Ikiwa amesimama nyuma ya kila neno alilotamka,basi inafaa tupate thibitisho kamili katika unabii ULIOTIMILIKU kuhusu Kanisa Lake.Huu ni UTHIBITISHO:

1.Je,Yesu aliomba-na hivyo AKATABIRI-kwamba Kanisa Lake litakuwa MWILI MMOJA,ulioungana katika utulivu kamili kama vile Baba na Yesu Mwana wa Mungu wameungana pamoja katika utulivu kamili? Yohana 17:20-23 na mstari wa 11.Je,Baba alikuwa akisikia maombi ya Yesu? Yohana 11:41-42.

**MAELEZO:**Mungu amekuwa akijibu maombi ya Yesu katika miaka 1900 iliyopita!Kanisa la Mungu ambalo Yesu alijenga-limekuwepo leo kama kundi MOJA LENYE UTULIVU la Waristo waliokombolewa na Roho,unaouunda "Mwili wa Kristo." (Uliza kitabu chetu cha Historia inayoendelea ya Kanisa la Mungu ili uone thibitisho la ajabu!)

2.Basi kwa nini kuna madhehebu mengi? Kama Mungu amekuwa akijibu maombi ya Yesu,kwa nini kuna makanisa TOFAUTI-wanaochanginyikiwa na hawana utulivu? Je,haya makanisa yanaweza kuwa sehemu ya KANISA LA KWELI ambalo Yesu alisema atalijenga? Ama ni makanisa ya ulimwengu huu YANAYOJIFANYA kama Kanisa la Mungu? Je,makanisa haya yanayokinzana NI SEHEMU YA ULIMWENGU HUU? Je,wanahusika katika siasa? Harakati ya mageuzi?Je,wamefuata desturi za ulimwengu huu? Je,Kanisa la Yesu

lingekuwa SEHEMU YA DESTURI YA ULIMWENGU HUU NA NJIA ZAKE? Yohana 17:14-16.

3.Basi mchafuko huu ulichipuka wapi-makanisa haya ya mafarakano yanayodai kuwa Wakristo walitokea wapi? Je, Yesu alitabiri kuwa wahudumu wa uongo WATAINGIA katika Kanisa la ukweli? Mathayo 7:15.Je,Petro pia alionya watu kuhusu walimu wa uongo ambao watajiingiza kanisani pasipojulikana ili walete uharibifu? 2 Petro 2:1-3.Je,walikuwa tayari wameaingia kanisani wakati wa Yuda? Yuda 3,4.Lakini,je walifukuzwa wakati Yohana aliandika? 1 Yohana 2:18-19.Kumbuka kwamba Biblia inaonyesha waziwazi kwamba wahudumu hawa waongo HAWAKUWA SEHEMU ya Kanisa la Ukweli Yesu alianzisha!

### **Nini ilifanyikia Kanisa la Awali iliyoleta Mkondo huu wa Wakristo wa Kisasa?**

Wakati tuna kitabu kinachoeleza kwa undani kinachoitwa *Historia Inayoendelea ya Kanisa la Mungu* (Kinapatikana bure kwa mtando [www.c cog.org](http://www.c cog.org)) maelezo mafupi yanaweza kusaidia hapa.

Yesu alifundisha kwamba Kanisa la kweli litakuwa "kundi dogo" (Luka 12:32), kuchukiwa na ulimwengu (Mathayo 10:22), na kuteswa (Mathayo 10:23). Alifundisha kwamba wachache watapata njia ya uzima wa milele kwa wakati huu (Mathayo 7:14,20:16). Mtume Yuda anaonyesha kwamba idadi ya watakatifu ni wachache (Yuda 14), na Mtume Paulo aliwaita kundi hilo "mabaki" (Romans 11:15). Katika karne ya kwanza, mtume wa uongo anayeitwa Marko (Siye Marko aliyeandika kitabu cha Marko), alihubiri istiari ya tafsiri ya maandiko katika Aleksandria. Aleksandria ulikuwa kituo cha kitaaluma kilicho julikana sana cha Utawala wa Rumi hapo zamani na ulikuwa mji ulio na ushawishi mkubwa sana katika ulimwengu wa Wagiriki-Warumi. Kilichopewa mada ya uongo "Nyarakaza Barnaba" kilitoka Aleksandria katika mwanzo wa karne ya pili na pia akahubiri istiari ya tafsiri za maandiko (Tazama malango wake wa 10:2). Wapingaji na waasi Valentino na Basilida walikuwa watu wa Aleksandria. Katika urogi wa karne ya tatu (Isaya 47) na uliodaiwa kama ujumbe wa "Mariamu" uliathiri wengi. Katika utawala wa Kirumi dhehebu ya Mithra ilikuwa inaenea sana wakati toleo la Ukristo pia lilikuwa. Wengine walidhani kuwa madhehebu

hayo yalikuwa yakishindana (Hata hayo yalikuwa mashindano ya walegevu na wafuasi wa Mithra). Mithra alikuwa ni mungu wa pagani wa jua. Imani nyngi na vitendo vinavyohusiana na Mithra vilianza kugusa wengi waliodai kuwa watangazaji wa Kristo kuanzia karne ya pili mpaka karne ya nne.

Kulingana na mwanahistoria wa karne ya 18 E.Gibbon, mnamo 135 B.K, wengi waliodai kuwa Wakristo kule Yerusalem walichagua kuongozwa na kiongozi wa kilatini Markas ambaye aliwashauri kulegeza sheria za Mungu (ambazo Gibbon aliziita, "Sheria za Musa") ili kukidhiwa na Mtawala wa Rumi aliyeitwa Hadrian. Ulegevu mwingine ulianza kufanyika wakati huo, kwa sababu hiyo ya kukidhiwa.

Makubaliano ya mafundisho ya waasi wengine (kama vile Simoni Magusi, Masioni na Montanasi) yalienea kwa wale wanaodai kuwa Wakristo. Waasi wengi walifundisha istiara, kama vile Valentino, alitoka Aleksandria mpaka Rumi na mahali pengine na kuanza kufundisha siri na ukweli kidogo. Na wakati historia inaonyesha kwamba viongozi wa karne ya pili kutoka Asia Ndogo walipinga hawa waasi na mafundisho yao, wengi walivumiliwa, angalau kwa miongo, na makanisa makuu katika Rumi na Aleksandria. Sababu ya kuyakubali mafundisho ya waasi ni kwamba yalikuwa yanaongeza idadi ya watu wa mataifa katika makanisa hayo.

Tazama alichoandika mwanahistoria mmoja:

Uasi ukichanganywa na imani ya Kristo wengi wanaadhimu kwenye mafundisho ya giza... Waasi waligawanyika kwa zaidi vikundi hamsini visivyoelewaka ambavyo vilivyosherekewa sana vilikuwa Wabasilida, Wavalentino, Wamaisoniti. ..kila kikundi wangejivunia maaskofu wao na usherika wao, madaktari wao na wafia dini wao, na badala ya Injili Nne zilizofuatwa na kanisa, waasi walitengeneza historia nyngi na mahubiri ya Kristo na mitume wake zilizorekebishwa katika kanuni yao. Mafanikio ya Waasi yalienda haraka na ya kina. Walienea Asia na kuwa imara katika Rumi, na pia wakati mwingine kuingia mpaka mikoa ya Magharibi. Katika sehemu nyngi, waliibuka katika karne ya pili...

Watu wa mataifa waliobadilika,ambao upingaji wao na dhuluma yao ilielekezwa dhidi ya sheria ya Musa,wangepata ruhusa ya kuingia katika mashirika mengi ya Wakristo,ambayo hayakuhitaji kutoka kwa mawazo yao yasiyofundishwa,imani yoyote ya ufunuo uliotangulia.Imani yao iliimarishwa na kukuzwa,na Kanisa hatimaye lilifaidika na ushindi wao wa nguvu kwa maadui yao (Gibbon E.Decline and Fall of the Roman Empire,Volume III,Chapter XXVII,ca.1776-1788).

Wakati hatukubaliani na Gibbon ya kwamba kanisa "hatimaye lilifaidika" kutoka kwa ulegevu huu vile inavyodokezwa,ulegevu huu uliruhusu mwelekeo tawala wa makanisa ya Wagiriki-Warumi "kuongezeka" vile Gibbon alivyoandika na wakawa wengi ya waliokiri Kristo.

Hata hivyo wengi wanaonekana kukubali mchanganyiko wa mawazo ya Wapagani na Ukristo,hiyo siyo njia inatakikana ifanyike.Kumbuka ,kwa mfano,utimizaji wa unabii wa Nehemia:

30 Hivyo nikawatakasa na kila kitu kigeni.(Nehemia 13:30)

Hata hivyo,wengi waliokiri Yesu katika karne chache za kwanza hawakushirikisha mtazamo wa Nehemia kwa vile waliweka dhana ya pagani kwa imani yao.Yesu mwenyewe alionya kuhusu kuitisha vitendo vya pagani katika maombi (Mathayo 6:7).Wakristo hawapaswi kuwa na "roho ya ulimwengu" au kupenda vitendo vyake (1 Yohana 2:15).

Licha ya maonyo ya Biblia,katika karne ya pili,shule moja au nyingi zilibuniwa za waasi katika Aleksandria,pamoja na shule iliyongozwa na mwasi-nusu Klementi wa Aleksandria na baadaye Orijeni.ambaye mafundisho yake yalisawisha wanaokiri Kristo katika ulimwengu wa Wagiriki-Warumi.Hata hivyo,mafundisho mengi ya shule hizo yalikuwa yamekemewa kama uzushi,hata na Wakatoliki na vyanzo vya Protestani-ingawa wengi walikuwa na mshikamano wa kipani,wengi waliokiri Ukristo bado walishawishika nazo.

**MAELEZO:**Biblia inaonya kuhusu WAONGO ambao wanaingia kwa siri Kanisani chini ya

uongo wa KUJIFANYA.Walijifanya kuwa-na kuonekana kama kondoo.

Hawa kondoo waliovaa ngozi ya kondoo walijaribu kuingia katika Kanisa la kweli,walichukue,KUBADILISHA na kuingiza mafumbo yao ya Kibabeli badala ya mafundisho ya ukweli ya Mungu na torati,na bado kulifanya liwe kama Kanisa la kweli la Kristo!! Ulikuwa msukumo wa kishetani wa harakati ya pagani iliyowekwa kupiga muhuri jina la Kristo kwenye dini ya ulimwengu ya pagani!

Mtume Paulo aliwaita,kwa HAKIKA,watumishi wa Shetani ( 1 Wakorintho 11:14-15).Bado walijiita mitume wa Kristo lakini walikuwa mitume wa UONGO (Mstari wa 13).

Wakati Yuda aliandika,mnamo mwaka wa 67 B.K.,walikuwa tayari wameingia kwa siri na kujifanya kwa uongo,wakigeuza NEEMA kama LESENI ya kutotii Amri za Mungu (Yuda 4).Katika nyaraka zao,Yakobo na Petro walizungumza kuhusu upinzani dhidi ya Amri za Mungu.Mtume Yohana alikumbana nayo katika nyaraka zake alizoandika katika miaka ya 90 B.K.Wakati huo hawa walaghai walikuja na KUENDA! Lakini walidai kwamba WAO,na wafuasi wao,SILO Kanisa la Mungu la kweli,walikuunda "Ukristo" awali na Kanisa la awali la ukweli.Lakini HAWAJAKUWA SEHEMU ya Kanisa la Kweli ambalo Yesu alianzisha! (1 Yohana 2:19)

4.Je,walimwengu walianza kusikiliza uzushi na hekaya ya walimu waongo,badala ya kusikiliza ukweli wa Mungu? 1 Yohana 4:5.Je hii ni ukweli kwa ulimwengu wa leo?

5.Je,Yesu alitabiri kuwa WENGI leo,sio wachache,watadanganywa? Mathayo 24:4-5 na Marko 13:5-6.Luka 21:8 inasema nini? Je,wengi –ama WACHACHE-wanapata njia ya amani inayoongoza kwenye uzima wa milele? Mathayo 7:13-14.Je,hii pia inaonekana kwamba wengi wanaokiri kuwa Wakristo ni wa Kanisa la ukweli la Mungu leo? Je,unabii huu wote unaonyesha ya kwamba WENGI WAKATI HUU wametegwa na Babeli ya wanaokiri dini za "wakristo"?

**MAELEZO:**Katika unabii wa Yesu kwa LEO alitabiri juu ya watumishi wa uwongo-na "makanisa"yao ya uwongo-watakaokuja kwa jina lake,wakijifanya kama watumishi wa ukweli wa Kristo,wakikiri Ukristo,huku

WAKIKANA ujumbe Yesu aliuleta kutoka mbinguni.

Ukweli huu unaeleza vile maarifa ya ukweli yamepotea kwa ulimwengu na UMEHIFADHIWA na Kanisa la Mungu la ukweli.Kwa sababu Kanisa la Mungu PEKEE LINAISHI kwa kila neno la Mungu,wakigundua na kuwasilisha mamlaka kuu ya Kristo juu ya washirika wake kwa jumla!

6.Hata kama ulimwengu ungeweka ujisadi kwenye ukweli-hata kama walikubali JINA LA KRISTO-Je,Yesu ALITABIRI kwamba Kanisa lake litahubiri habari njema ya Ufalme wa Mungu katika nyakati za mwisho wa dahari? Mathayo 24:14.

7.Je,Kanisa la Mungu—"Kanisa la Mungu Linaloendelea"—linahubiri habari njema kutoka kwa makao yake makuu ya California? Je, Kanisa la Kristo pia linatekelezwa kwa nguvu na fedha ya ulimwengu? Ama liko na "nguvu kidogo" ambayo MUNGU ANASUKUMA ili itumike kwa MAARIFA katika NJIA KUBWA kuhubiri ujumbe wa maonyo ya Kristo kwa ulimwengu? Ufunuo 3:8.

**MAELEZO:**Kuwepo kwa Kanisa la Mungu la Ukweli leo pia ni thibitisho kwamba Mungu Yupo!

Haya ni baadhi ya maandiko zaidi ya MIA ambayo yanadhihirisha bila shaka kwamba ALIOTABIRI YESU KWAMBA ITAFANYIKA kwa Kanisa lake INAFANYIKA LEO! Na ulimwengu umegeuzwa kwenye hekaya ambazo zinazojifanya kama "habari njema ya ukweli" VILE YESU ALIVYOTABIRI!

Historia inaonyesha kwamba Kulikuwako na makundi yaliyokiri Kristo katika karne ya pili/tatu na nne.

Kundi moja lilikuwa lile lililodai watakatifu wa Wagiriki-Warumi (Othodoksi na Katoliki wa Rumi) kama vile Polycarp wa Smirna,Thirasis wa Umenia,Apolonia wa Efeso na Apolinaris wa Hiropoli,Serapino wa Antiokia,na Neposi wa Afrika Kaskazini.Wale walioko katika kundi hili walidai mafundisho/utendaji kama vile Pasaka ya tarehe 14,kutokula nyama chafu,Sabato,uungu mbili,millennia,kanuni nzuri ya Agano Jipy,a kutoshiriki katika jeshi,na kuamini katika maandiko.Walielewa na kuendeleza habari njema.

Kundi lingine lilijumuisha wengi waliouwa na kuamuru mateso.Kundi hili ni la waliochanganya fikra za siri ya

uasi,fumbo,Umithra na kuupuzia unabii mwengine na maelezo yao ya "Ukristo".Walijaribu kuidhinisha injili ingine. Makundi haya yote yalikuwepo katika karne ya pili,ya tatu na ya nne.katika karne ya pili,kundi la kwanza lilidhihirika kuwa kubwa mpaka baada ya ulegevu na mateso,kundi la pili likafanikiwa katika maeneo mengi (Tazama pia kitabu chetu cha *Historia Inayoendelea ya Kanisa la Mungu*).

Makundi haya yote(na sehemu zao tofauti) yamekuwepo katika vipindi hivi vyote.

Makundi haya yote yamekuwepo leo.

Moja (Wagiriki-Warumi) wanafundisha kwamba makundi haya yote yalikuwa sehemu yao.Lingine (Kanisa la Mungu la kweli) linafundisha kwamba moja kati ya makundi mawili walikuwa waaminifu,na wanafuutilia mafundisho hayo pekee yake.

8.Je,Yesu alifundisha kwamba kutakuwako na makundi mawili na kwamba kundi la ukweli litakuwa ya watu wachache? Mathayo 7:13-14;Luka 12:32.

Sasa,wengi,kulingana na Yesu,watajipata katika makundi mabaya na wachache watapatikana kwa kundi halisi ya Wakristo.

9.Je,Mtume Paulo alifundisha fundisho sawa kuhusu kipindi hiki? Warumi 11:5.

Ni Kanisa halisi la Mungu ,linalowakilishwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG),linadai kuwa na mshikamano na Mtume Yohana na orodha ndefu ya mafundisho na viongozi,pamoja nay ale yaliyoorodheshwa katika somo hili.Viongozi amba walichukua nafasi ambazo makanisa ya Wagiriki-Warumi wanadai ni wazushi.

Wengi wa makundi mengine wanaodai kuwa Wakristo,kwa wazi au kwa siri wana mshikamano na kundi la waistiari( na walikubaliana na maamuzi mengi,bali siyo yote ya baraza ya awali kabla ya 700 B.K.) ama kimsingi wanataka kufanya kana kwamba ni waamini hata hivyo hawakutoka kwenye makundi hayo mawili ambayo makala haya yanajadili.

Kwa vile Yesu aliweka wazi kwamba Kanisa lake mwaminifu litakuwa "Kundi dogo" (Luka 12:32) ambalo haliwezi kufa ama kuangamizwa (Mathayo),kundi la watu wachache amba walitoka kwa kundi la awali ndilo kanisa la ukweli.Kanisa hilo linaashiriwa na Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).

10.Je,Yesu pia alitabiri wakati ambapo Mungu ataingia kati katika shughuli za ulimwengu na kukomesha vitisho vinavyokaribia ya maangamizo ya maisha ya wanadamu? (Mathayo 24:21-22).(Tulizungumza haya katika somo la Kwanza ya Kozi hii)

**MAELEZO:**Hapa pia tunaona thibitisho kwamba Mungu yupo! Alijua kabla-akapanga matukio ambayo yanatukia tukiona kwa macho yetu.Yeye ndiye anahusika na vichwa vya habari tunavyosoma kila siku-VICHWA VYA HABARI AMBAVYO VINAASHIRIA UTIMIZAJI WA HARAKA YA UNABII ULIOSALIA MARA BAADA YA HABARI NJEMA YA UFALME KUHUBIRIWA KWA ULIMWENGU WOTE KAMA USHUHUDA!

#### **Thibitisho la Tatu:Maarifa na Ongezeko la Idadi ya Watu Kutabiriwa**

Wengi hawaamini utimizaji wa kihistoria ya unabii wa Biblia.Wale wasiodai kuwa Wakristo hawajali ikiwa au jinsi Yesu alitimiza unabii wa kitambo.Wengi hawajali unabii unaohusiana na Kanisa la Kweli la Mungu.

Lakini kuna baadhi ya unabii ambao umetimizwa kuanzia wakati ambapo Agano Jipya liliandikwa ambao unafaa uwapatie wasioamini kusita wakifkiria ya kwamba mkono wa Mungu ulikuwa nyuma yao.

Kumbuka yafuatayo Danieli aliambiwa kuhusu siku za mwisho:

4 "Lakini wewe,Ee Danieli,yafunge maneno haya,ukikitie muhuri kitabu,hata wakati wa mwisho;wengi wataenda mbio na maarifa yataongezeka." (Danieli 12:4)

Safari za kisasa ni ya haraka sana kuliko vile Danieli alifikiria itakuwa kimwili.

Kwa uundaji na matumizi ya Kompyuta ya kisasa,na intaneti ,kumekuwako na ongezeko la maarifa ulimwenguni kote.

Je,utabiri huu ulikuwa kisio cha bahati?

Zingatia pia unabii mwingine wa nyakati za mwisho:

13 Malaika wa sita akapiga baragumu,nikasikia sauti moja iliyotoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyo mbele za Mungu.14 ikimwambia yule malaika wa sita aliyejkuwa na baragumu,Wafungue nao malaika wanne waliofungwa kwenye mto kubwa Frati.15 Wale malaika wanne

wakafunguliwa,waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka,ili kwamba wae theluthi ya wanadamu.16 Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa elfu ishirini mara elfu kumi;nilisikia hesabu yao.(Ufunuo 9:13-16)

Wakati unabii ulio juu uliandikwa,hawakuwepo watu milioni 200 kwenye sayari,wacha hata wanaume kiasi hicho cha kufanya jeshi ya idadi hiyo.Unabii huu,pia,ulikuwa wa nyakati za mwisho.

Biblia pia ilionya kuhusu ushirikiano wa jeshi na kijiografia na kisiasa ambao tunaona ukiundwa leo.

Hakuna mtu wa busara atayedhania kwamba unabii huu ni "kisio cha bahati" uliofanywa miaka 1900 iliyopita,haswa ukichanganywa na unabii mwingine ambao umethibitishwa.

#### **SOMO la Unabii**

Kabla hatujakamilisha somo hili ya *Kozi ya Biblia*,ni muhimu kuelewa ukweli moja mwingine.

Vile tumeeleza unabii uliotimilika kwamba Mungu Yupo,tunaletwa ana kwa ana na utambuzi kwamba Mungu ni Mtawala mwenye mamlaka.Kama Mtawala Mwenye Mamlaka anaamuru kujitoa usio na masharti kwake na KUTII KWETU KWA AMRI NA SERIKALI –na NJIA zake za maisha.Huu ndio UJUMBE WA MANABII WOTE TANGU ULIMWENGU UANZISHWE!

Manabii hawakuwa wenyewe mashauku ya kidini,wenye mageuzi ya madhehebu ya ulimwengu na maadili,ama wanasiwa ambao walikisia kuhusu siku zijazo ili kwamba washawishi ulimwengu wa wakati wao.Dhana hili ni wazo la kosa la watu wa kisasa na wanatheolojia wanaotazama mambo kimantiki.

Manabii walikuwa tu WALINZI ,WALEZI wa ukweli wa Mungu waliotumwa kuonya watu,miji,mataifa na ulimwengu kuhusu matokeo yanayoletwa na dhambi.Manabii walipokea funuo kutoka kwa Mungu wa rehemea na kuwapelekewa watu KABLA Mungu hajamwaga ghadhabu yake kwa watu na mataifa ambayo yanapinga mapenzi yake na wanaofanya kile wanachokiona kama ni vyema machoni pao.Walinzi wa Mungu wanaonya LEO! Wanaonya mataifa kujitoa kwa Mungu pekee ambaye anajua mazuri na mabaya.

UNABII UNAONYESHA ADHABU YAFAAYO Mungu anaahidi kutumia kwa sababu ANAPENDA wanadamu na ANATAKA WALETE HISIA ZAO. "Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote,bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake." (Amosi 3:7).Mungu anaahidi,kupitia unabii,kutupatia nafasi ya kutosha ya MAONYO ILI TUGEKE KWA NJIA ZA MUNGU ambazo ni za muhimu sana kwa binadamu.

Somo zima la unabii linapatikana katika 2 Wafalme 17:6-23:

"....Ashuru akautwaa Samaria...wakabeba Waisraeli mbali' Kwa nini? Waisraeli walikuwa wametenda dhambi juu ya BWANA na kuwaheshimu miungu mingine na kutembea katika desturi ya nchi zingine"wakachukua njia ya maisha iliyoonekana vyema kwenye mataifa yaliyowazingira....na bado BWANA ALIWAONYA WAISRAELI NA YUDA NA KILA NABII NA WANAO ONA"-Mungu aliongea kupitia kwa manabii na wale walioona njozi—"akisema geukeni,na kuziacha njia zenu mbaya,MKAZISHIKE AMRI ZANGU NA HUKUMU ZANGU,sawasawa na ile sheria yote nilioamuru baba zenu,NIKAWAPELEKEA KWA KINYWA CHA MANABII WATUMISHI WANGU"(Mstari wa 6-13).

Manabii wa Mungu walikuwa wanenaji wake,wakifunua amri zake kwa taifa lililoasi na kusahau.

"Walakini hakutaka kusikia,bali walifanya shingo zao kuwa ngumu,kama baba zao,wasiomwamini BWANA,Mungu wao.Basi BWANA akakikataa kizazi chote cha Israeli...kama vile alivyosema kwa kinywa cha watumishi wake wote,manabii" (mistari ya 14,20,23).

MANABII WALIWEKA WAZI SABABU ZA KINDANI ZA MAZINGIRA YA NJE.Walieleza MATUKIO YA ULIMWENGU katika uhusiano wa serikali na Amri za Mungu.

Hatima ya MAKUSUDI ya unabii ni kuleta mamlaka ya MAPENZI YA MUNGU mionganii mwa binadamu wote.Inatueleza LEO kwamba watu wengi hawataweza kujisalimisha kwa mamlaka na sheria za Mungu,Ataingia kati

mwenyewe katika shughuli za KUADHIBU WASIOTII na KULETA AMANI KWA MATAIFA. Kuwa makini ipasavyo kwa matukio ya unabii inasaidia mtu kuwa tayari kukaribisha Yesu (Luka 21:36).Zaidi ya hayo,ukweli wa unabii na matukio ya ulimwengu pia yanakusudiwa kuwa zoezi la kutafakari ili kwamba Wakristo wapate kutathmini maisha yao vizuri na kubadilika iwezekanavyo (Warumi 13:11-14;2 Petro 3:10-13).

Sababu nyingine ya kuwa makini na kusikiliza unabii na matukio ni kwamba usidanganywe na unabii wa uongo na mafundisho mengine.Hiyo ndiyo sababu tunayo afisi ya manabii:

11 Naye alitoa wengine kuwa mitume,na wengine kuwa manabii;na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu;12 kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu,hata kazi ya huduma itendeke,hata mwili wa Kristo ujengwe;13 hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu,hata kuwa mtu mkamilifu,hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;14 ili tusiwe tena watoto wachanga,tukitupwa huku na huku,na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu,kwa hila ya watu,kwa ujanja,tukizifua njia za udanganyifu.15 Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote,yeye aliye kichwa,Kristo.16 Katika yeye,mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo,kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.(Waefeso 4:11-16)

Kupitia miaka yote,watu tofauti wamedai kwamba mwisho u karibu sana kuliko vile uliviyokusudiwa.

Ya maarufu sana katika karne ya 21 ni matangazo ya aliyeaga Harold Camping.Lakini walioelewa matukio ya kisasa kulingana na unabii wa kiblia wangethibitisha kwamba alikuwa na makosa.

Kuna wengi ambao walikuwa kwa makosa na bado wengine wako kwa makosa.

Lakini haijalishi anayosema mtu ye yote, ulimwengu hautaisha mwaka huu, au mwaka ujao ama mwaka ule mwingine.

Nawezaje kuwa na uhakika?

Ni, vyema kwa sababu moja, Mtume Paulo aliandika:

19 Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo mkiangalia, mwafanya vyema (2 Petro 1:19)

Hili ndilo suala la Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG).

Sababu ya kutazama matukio na kuelewa unabii wa Biblia ni kwamba tusiathirike na wanaoendelea mafundisho ya uongo au wanadai kuwa mwisho unaweza kuja kabla Biblia haijaruhusu (2 Wathesalonike 2:2; Waefeso 4:14).

Unabii pia inatuhakikishia kwamba Mungu anatawala na atafanya mapenzi yake. Kwa hivyo waaminifu wasiogope wanaosema watu ama watakachofanya (Luka 12:32).

Biblia ni wazi kwamba matukio mengine yanafaa kutokea kabla mwisho ufike. Na hiyo inatufanya sisi tukue "Kwa imani na katika kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo" (2 Petro 3:18)

Sehemu ya maarifa hayo ni unabii. Na sehemu ya maarifa ya kibiblia inatuambia kwamba ulimwengu hautaisha kabla matukio ambayo Biblia inatueleza hayajafanyika kwanza.

Kwa nini unabii?

Ili tuwe macho, kimwili na kiroho na pia tuisiyumbishwe na wengine amba o hawana upendo halisi ya ukweli.

Wacha tuchunguze tena Warumi 3 kwa undani ili tuelewe KWA NINI Mungu ametabiri hukumu kwa ulimwengu huu wetu:

1.Je, ni kawaida kwa wanadamu kuelewa kusudi la maisha? Warumi 3:11, sehemu ya kwanza.

2.Je, binadamu bila uwezekano wa Mungu, kiasilia anaweza kutafuta Mungu na kumtambua? Mstari wa 11, sehemu ya mwisho. Je, hii pia inaonyesha wazi kwamba binadamu HAWEZI kutafuta Mungu ila tu AKIDHIHIRISHA PEKE YAKE? Je, hii ndiyo tulisoma kutoka kwa Somo la 9 ya Kozi hii?

3.Basi tazama mstari wa 12. Je, wanadamu wote wameenda kwenye njia waonayo kuwa ni nzuri kwoo? Je, Mungu anasema kwamba

wanadamu wamepotea kutoka kwenye njia yake?

4.Je, mstari wa 12 inaashiria kwamba Mungu AWALI alionyesha njia yake kwa binadamu na binadamu AKAPOTOKA kutoka kwa njia hiyo? Ni, jinsi gani wanaweza "KUPOTOKA wote"? Basi, je mataifa YAMEPOFUSHWA katika ujinga na ushirikina? Je, wanafaida yoyote kwao au kwa Mungu vile walivyo? Kama kawaida, uhakikishe umeandika jibu ya maswali haya kwenye daftari lako.

5.Wangapi kwa asili wanafanya vyema badala ya mabaya? Sehemu ya mwisho wa mstari wa 12. Ungeweza kusema kwamba ulimwengu umeamini hivyo?

**MAELEZO: WAASI NA WAKAFIRI** bila shaka WANAKATAA UNABII KWA SABABU HAWATAKI KUFANYA MAPENZI YA MUNGU! Wanataka kufanya mapenzi yao ambayo yanaleta maumivu ya moyo, mateso, magonjwa, vita na mauti! Wengine hawaamini yanawaathiri, hata kama wanadai kuamini Biblia.

Hata wenye msimamo thabitil amba wanakiri kumjua Mungu, WANADANGANYA, kwa sababu WANAKATAA KUFUATA AMRI ZAKE: "Yeye asemaye" Nimemjua", wala hazishiki amri zake ni MWONGO, wala KWELI HAIMO NDANI YAKE" (1 Yohana 2:4). Watu hawa WANAGEUZA maana ya unabii ili kwamba waendelee na mapenzi ya uasi dhidi ya amri za Mungu.

Haitoshi kugundua kwamba Mungu yupo. Unabii unathibitisha kwamba pindi tumegundua kuwepo kwake, tuna wajibu wa KUGUNDUA MAMLAKA YAKE na KUYATII mapenzi yake ambayo ameonyesha katika Torati, amri na hukumu zake!

Pia inafaa itajwe kwa sababu Wakristo wa ukweli wengi hawaungi mkono kazi ya ukweli ya Mungu katika nyakati za mwisho, kwamba hawataelewa kinagaubaga unabii muhimu, licha ya wanayoambiwa na viongozi wao wa Laodikia (Ufunuo 3:14-22) na sardi (Ufunuo 3:1-6).

Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili, ambalo Roho ayaambia makanisa. (Ufunuo 2:7, 11, 17. 29; 3:6, 13, 22).

Mara saba katika Ufunuo, Yesu haswa anawaambiwa wale washirika wa Kanisa la Mungu la ukweli wawe makini na ujumbe kwa makanisa. Wingi wa utabiri huu ulikuwa unabii na marekebisho.

Bado hata Wakristo wengi hawaelewi vizuri alichosema Yesu ama kuelewa vizuri ukweli kuhusu unabii ambao utawaathiri katika karne ya 21.

### Mungu


Sasa unao uhakika kwa ufupi-ukweli ambao unathibitisha kwamba Mungu LAZIMA AWEPO.Lazima awepo ili awatia msukumo watu walioandika Biblia karne nyingi zilizopita. Lazima azidi kuwepo na kutawala juu ya mataifa ili kwamba alete unabii kwa utimizaji! MUNGU ANAYEISHI NA KUTENDA anaweza kukomesha wasioamini na makafiri kufanya alichosema tusifanye!

Hata nguvu zote za Muungano wa Mataifa haiwezi kujenga alichosema Mungu "tusijenge."

Unabii huu wote haungeandikwa baada ya matukio haya kuyatukia.(Tumewacha kimakusudi unabii ambao wakanaji wanadai KWA UONGO kwamba uliandikwa BAADA ya tukio lenyewe.)

Manabii walioandika Biblia wamekufa.Hawangetimiza maandiko yao.Mungu anayeishi,mweza yote ndiye angeingia kati kwa karne hizo kuleta kila unabii kwenye utimizaji bila kuuwacha wowote! HAKUNA UNABII AMBAO HAUJAFALU!

### Yupo!



### Vidokezi Ishirini na Nane vya Maombi Yanayofaa:Sehemu ya 5

Na Bob Thiel

*Hii ni sehemu ya tano ya sehemu nyingi mfululizo kuhusu maombi.*

Imesemekana kwamba, "Kanisa la Mungu linaenda mbele kwa kupiga magoti."msemo huu umekuwa ukitumika kama himizo kuwaambia Wakristo kwamba wanapaswa kuomba.Lakini kwa namna gani?

Katika makala yaliyopita,maombi yalifafanuliwa na vidokezi ishirini na moja kujadiliwa.Katika makala haya,vidokezi vingine vitatu,kuanzia na kile tunachoita kidokezi ishirini na mbili kimejadiliwa.

### Kidokezi 22:Waombee Viongozi wa Dunia

Katika Agano la Kale,viongozi wengine waliuliza watu wa Mungu wawaombee,na wakafanya hivyo (1 Wafalme 13:6;Ezra 6:8-9). Na,je katika Agano Jipy? Wakati wengine wanaamini kwamba shida wanadamu wanakumbana nazo zitatuliwa kwa njia ya kupiga kura ama ghasia,Biblia inasema inatupasa kuwaombea viongozi wa kawaida na wale walioko katika serikali ambao wana mamlaka juu ya vipengele vya maisha yetu.

1 Basi,kabla ya mambo yote,nataka dua,na sala,na maombezi,na shukrani,zifanyike kwa ajili ya watu wote;2 kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka,tuishi maisha ya utulivu na amani,katika utauwa wote na ustahivu.3 Hili ni zuri,nalo lakubaliwa mbele za Mungu Mwokozi wetu ( 1 Timotheo 2:1-3).

Wengi wetu tunakumbana na matatizo na maafisa ya serikali na sera zao.Je,unawaombea vile upasavyo? Kwa vile mambo ya serikali ya kimataifa yanavyoenda,Biblia pia inasema, "waombeni Yerusalem amani (Zaburi 122:6).

**Kidokezi 23:Weka Yesu katika Maombi Yako**

Kuna jina moja tu chini ya mbingu ambao tunaokolewa kwalo:Yesu (Matendo 4:10,12).Tunapaswa kuweka Yesu kwa maombi yetu.Haya hayamaanishi kwamba tupeleke maombi kwa Yesu,hata hivyo hiyo inawezafanywa (k.v Matendo 7:59),inatupasa kugundua kwamba tunaweza kuja kwa Baba kwa sababu ya yale Yesu ametutendea.

Kitabu cha Waebrania kinatufundisha:

14 Basi,iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu,Yesu,Mwana wa Mungu,na tuyashike sana maungamo yetu.15 Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu;bal yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote,bila kufanya dhambi.16 Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri,ili tupewe rehema,na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.(Waebria 4:14-16)

Tunafaa,na inatupasa,tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri,kwa sababu ya Yesu.

Tazama pia alichoandika Yesu:

13 Ninyi mkiomba lolote kwa jina langu,hilo nitalifanya,ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.14 Mkiomba neno lo lote kwa jina langu,nitalifanya.(Yohana 14:13-14)

Je,kuna mipaka? Kumbuka

alichoandika Mtume Paulo:

13 Naweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.(Wafilipi 4:13)

5 Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.(Wafilipi 2:5)

1 Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.(1 Wakorintho 11:1)

Ikiwa umetubu,umebatizwa,na kupokea Roho Mtakatifu wa Mungu,damu ya Yesu imekuosha safi (Ufunuo 1:5).Utakapofuata Yesu kwa ukweli,utawenza mambo yote kupitia kwake.Jaribu uwe na ufikirie kama Yesu.

Mtume Yohana aliandika:

23 Amin,amin nawaambia,Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu.(Yohana 16:23)

Kwa sababu ya kujitolea kwa Yesu,inatupasa tuombee,tukiuliza Baba,katika jina la Yesu/mamlaka yake.Huwa ninamalizia maombi yangu kwa kuomba yale niliyoombea kwa jina/mamlaka ya Yesu,kulingana na mapenzi ya Mungu.Yesu ndiye mpatanishi kati ya binadamu na Mungu (1 Timotheo 2:5):Usiombe kwa au kupitia kwa mama yake ama mwingine.

Mengi kuhusu maombi yanaweza kupatikana katika kitabu chetu cha *Maombi:Biblia Inafundisha Nini?*

Kuitekeleza Mathayo 24:14

Pamoja na Mathayo 28:19-20



Kanisa la Mungu Linaloendela (CCOG) [www.ccog.org](http://www.ccog.org)

Taarifa za unabii wa Biblia za Kilasiku: [www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)

CCOG.ASIA: Hii ni Tovuti ilengayo wasomaji kutoka Asia.Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za kiasia.

CCOG.EU: Hii ni Tovuti kwa wale wa Ulaya.Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.

CCOG.IN: Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Kihindi.

CCOG.NZ: Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya New Zealand.

CCOGCanada.CA: Hii ni Tovuti inayolenga walio wa asili ya Canada.

CDLIDD.ES: Hii ni ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) katika lugha ya Kihispania.

PNHIND.PH: Hii ni Tovuti kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.



**Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia:**  
[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](http://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)

**Chaneli ya Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG):**[www.youtube.com/continuingcog](http://www.youtube.com/continuingcog)

Mchungaji Mwandumizi wa Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) ni mgeni mwalikwa mara kwa mara kwenye radio, akitumia radio kuwafikia wasikilizaji wa maeneo mengi. Kanisa la Mungu Linaloendelea (CCOG) pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielektoniki, vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika kutekeleza  
Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19-10

